DIWANI YA HADITHI ZA WATOTO

Juzuu ya 5

Hadithi Fupi 22 za Kiswahili

Hadithi zaidi zinapatikana:

African Storybook.org

Kimechapishwa na:

Elimu Yetu

Soma zaidi:

maktaba.org

Diwani ya Hadithi za Watoto
Juzuu ya Tano

Yaliyomo:

Aku Rafikiye, Jua	3
Anansi, Kunguru na Mamba	17
Anansi na Kasa	30
Anansi na Tai	42
Demane na Pacha Wake	56
Familia ya Pembenyingi	88
Hakimu asiyekuwa na Busara	106
Jambazi	128
Kumsubiri Mtoto	146
Mamba aliye Mwilini Mwangu	160
Matunda	173
Mbweha na Jua	187
Mti Ulionusuru Kijiji cha Balantu	199
Mwalimu Goso	215
Ndalo na Pendo – Marafiki Wakubwa	232
Ndege Asali Alipiza Kisasi	246
Ndizi za Bibi	263
Refi Awaosha Kuku Wake	275
Samaki Mkarimu	300
Tembo Mdogo	318
Theuri Amwokoa Kobani!	326
Uamsho wa Furaha	339
Wakati Basi Kubwa la Bluu Lilipochelewa	348
Wanamuziki Stadi	366
Wanyama Hushukuru	375
Zawadi ya Sisanda	394

Aku, rafikiye Jua

Ursula Nafula
Idowu Abayomi Oluwasegun

Kiswahili

African Storybook.org

Hapo zamani, kuliishi msichana mmoja katika kijiji kilichoitwa Nchijua. Msichana huyo aliitwa Aku. Alikuwa msichana mwenye miguu mirefu mno.

Aku alistaajabishwa na mambo mengi.

Babake Aku aliitwa Juma na alikuwa mvuvi. Wakati mwingine, Juma alienda na Aku kuvua samaki. Alipofanya hivyo, Aku alistaajabu kwa nini kila mara jua lilimtazama kutoka juu angani.

Mara nyingine Aku alimsaidia mamake, Agatha, kupika. Alipofanya hivyo, alistaajabu kwa nini mafuta yalikuwa rangi nyekundu yalipokuwa kwenye kibuyu lakini kuwa manjano yakiwa kwenye viazi vikuu.

Pia, Aku alistaajabu kwa nini Oti, kakake, na wavulana wengine hawakumruhusu acheze nao mpira wa miguu. Aku alipowauliza kwa nini, walicheka kisha wakamwambia aende acheze na wasichana wenzake.

Wasichana nao hawakutaka kucheza naye. "Miguu yako ni mirefu sana," walimwambia Aku kila mara.

Aku alifanya urafiki na jua. Alitazamia kuliona jua kila alipoamka asubuhi. Jogoo walipowika kutangaza mawio, Aku alichezea juani huku kivuli chake kikicheza naye. Kuimba kwa ndege na kuwika kwa jogoo ilikuwa muziki mtamu kwake. Jua lilimfurahisha na kumfanya atabasamu.

Lakini siku moja, jua halikuchomoza.

Aku alisubiri jogoo kuwika, lakini, hawakufanya hivyo. Ndege hawakuimba. Bila jua, watu wa Nchijua hawakutekeleza majukumu ya kila siku. Wakulima hawakukuza mimea yao. Anga liligeuka kijivu likahuzunika. Juma hakwenda kuvua samaki. Watoto hawakwenda shuleni. Wanawake hawakujadiliana bei za bidhaa sokoni.

Aku alivikosa vitu hivyo vyote. Alikosa kuwika kwa jogoo na nyimbo walizoimba ndege. Alichokikosa zaidi, ni kuchomoza kwa jua.

Kila mmoja alitaka kujua jua lilienda wapi. "Labda jua limefariki," baadhi yao walisema. "Jua limesafiri," wengine wakasema. Wengine walimcheka Aku.

Hata hivyo, Aku alijipa moyo, "Ninasema ukweli. Jua ni rafiki yangu. Jua halijafariki." Lakini hakuna yeyote aliyemsikiliza zaidi. Walisahau jua wakamcheka Aku kwa nguvu. Kilichomhuzunisha zaidi ni kule kuchekwa na watoto wenzake.

Akiwa amehuzunika kama vile jua lilivyokuwa, Aku alifanya hima akaenda nyumbani. Aliugonga mpira wa kakake kimakosa. Mpira uliviringika na kuingia jikoni.

Mpira ulikigonga kibuyu cha mafuta kilichokuwa jikoni kikaanguka chini. Mafuta yalimwagika nao mpira ukaloa.

Oti na rafikiye mmoja waliingia jikoni kuuchukua mpira wao. Walikiona kibuyu kilichokuwa kimeanguka na mafuta yaliyomwagika. Mpira wao uliokuwa umeloa.

Oti, Agatha na watu wote wa Nchijua walimtazama Aku akitoroka. Walistaajabu wasijue alichopanga kuufanyia mpira ulioloa mafuta.

Aku alisimama alipofika katikati ya uwanja. Akauweka mpira chini na kwa nguvu zote, akaugonga kwa mmoja wa miguu yake mirefu. Mpira ukazunguka chini ukaelekea mwishwo wa uwanja. Ukaugonga mizizi ya mtende mmoja uliokuwa mwisho wa uwanja.

Mpira huo ulielekea angani. Wakiwa vinywa wazi, watu wa Nchijua waliutazama mpira ukiruka mbali na mawingu, mbali na upeo wa macho yao. Kila kitu kikatulia. Kukawa na kimya kikubwa. Ghafla, anga lilifunguka. Mawingu yakawa kama pamba nyororo. Mpira mkubwa ukapenyezea nyuma ya mawingu.

Mpira huo uliokuwa mwekundu na manjano kama mafuta, ukang'aa. Mpira huo ulikuwa jua, rafikiye Aku. Kila kitu kilisisimuka. Kimya kikamalizika.

Kila mtu alifanya hima kwenda nyumbani kujitayarisha kwa shughuli za kawaida. Juma alitafuta ndoo yake ya samaki. Wakulima waliyachukua majembe yao. Watoto walioga na kuvaa tayari kwenda shuleni. Wanawake walijifunga kanga zao. Walibeba vikapu wakaenda haraka sokoni.



Jua lilirejea Nchijua. Aku alikuwa amefaulu. Siku mpya ilianza...

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Aku, rafikiye Jua

Author - Aisha Nelson
Translation - Ursula Nafula
Illustration - Idowu Abayomi Oluwasegun
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2018
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org

Anansi, Kunguru na Mamba

Mutugi Kamundi
Wiehan de Jager

Kiswahili

African Storybook.org

Wakati mmoja kulikuwa na kiangazi na njaa kubwa. Hakuna aliyekuwa na chakula isipokuwa Kunguru.

Kila asubuhi walikwenda mbali katikati ya mto kwenye mkuyu uliokuwa na matunda matamu. Kisha walirudi wakiwa wamebeba makuyu hayo kuwaletea ndugu zao.

Alipoyaona matunda hayo, Buibui Anansi, alidondokwa na mate. Je, angewezaje kuyapata matunda hayo?



Baada ya kufikiri kwa muda mrefu, alipata wazo zuri. Alijipaka nta inayonata kwenye sehemu yake ya nyuma. Kisha akachukua kigae cha nyungu akaenda nyumbani kwa Kunguru akasema, "Tafadhali, naomba usadizi! Naomba kaa la moto. Jiko langu limezimika."

Walipokuwa wakimchukulia kaa la moto kutoka jikoni, Buibui Anansi alikalia kuyu moja kubwa. Tunda hilo lilijinata kwenye makalio yake. Aliwashukuru kunguru akaenda haraka nyumbani kulifurahia tunda hilo.

Lakini, tunda moja halikumtosha. Alirudi huko akafanya alivyofanya mara ya kwanza. Aliporudi mara ya tatu, kunguru walimwuliza. "Kwa nini unarudi hapa kila mara kuomba kaa la moto?"

Buibui Anansi akajibu, "Kila ninapofika nyumbani, kaa huwa limezimika." Kunguru walimwambia, "Unatudanganya! Unatamani chakula chetu." Buibui Anansi alijitetea, "Si kweli." Akaanza kulia. Wakamhurumia wakasema, "Beba kaa jingine. Asubuhi, tutakuonyesha mkuyu wenye matunda."

Asubuhi iliyofuata kila kunguru alimchangia Anansi manyoya akapata mabawa. Akaruka hadi kwenye mkuyu uliokuwa katikati ya mto.

Alipoona matunda yale matamu aliyataka yote peke yake. Kila wakati kunguru alipojaribu kuchuma tunda, Buibui Anansi alisema, "Wacha, hilo ni langu! Mimi nililiona kwanza!"

Halafu alichukua kila tunda na kuliweka mfukoni kwake. Hatimaye, alichukua matunda yote akawaacha kunguru bila chochote.

Kunguru waliyachukua manyoya yao. Buibui Anansi aliachwa peke yake.

"Siwezi kuishi kwenye mti huu maisha yangu yote," alijiambia. "Ni lazima niruke hewani kama kunguru."

Akashusha pumzi, kisha akaruka, na mara, chubwi! Akaanguka mtoni baina ya mamba hatari.

"Hapa tuna nyama tamu na nyororo." Mamba mmoja alisema. "Hebu tuanze kula mlo."

"Tafadhali, msiniue," Buibui Anansi akasema. Kisha akaanza kulia. "Kwani hamjui mimi ni mmoja wenu? Nilipotea wakati wa mababu zenu na hakuna aliyeweza kunipata. Sasa nyinyi ni ndugu zangu!"

Alilia machozi hadi mamba wakamwonea huruma.

Mamba mmoja mzee hakuamini, "Tutajua kwamba wewe ni mmoja wetu ukinywa supu ya matope kama sisi." Walimpatia kibuyu cha maji machafu. "Bibi yangu alikuwa akitengeza supu kama hii," Buibui Anansi alisema.

Lakini, alichimba shimo ardhini akitumia mguu wake wa nyuma, kisha akatoboa shimo kwenye kibuyu kwa mguu wake wa mbele. Alijifanya kwamba alikuwa akinywa yale maji na kumbe yalikuwa yakimwagika. "Tamu sana!" alisema huku akirudisha kibuyu kitupu.

"Sasa tumejua bila shaka kwamba wewe ni mmoja wetu," mamba wakamwambia. Walimruhusu Buibui Anansi kulala pamoja nao usiku huo.

"Kesho asubuhi nitawaambia hadithi kuhusu maisha yangu," Buibui Anansi aliwaambia walipokuwa wakianza kulala.



Siku iliyofuata, Buibui Anansi aliamka asubuhi na mapema akamwamsha mamba mmoja.

"Ningependa kwenda ili nimlete mke na watoto wangu ili wanisaidie kuhadithia. Je, utanisaidia niende kuwaleta kabla ya wengine kuamka?"



Mamba huyo hakufurahi kwa kuamshwa mapema sana. "Tafadhali nisaidie! Wewe unajua kuogelea haraka kuliko mimi," Buibbui Anansi akamwambia.

Mamba akakubali kumbeba Buibui Anansi kwenye pua lake hadi ukingo wa mto. Buibui Anansi aliposhuka kutoka kwenye pua la mamba alisema, "Nitarudi hivi punde. Tafadhali ningoje papo hapo!"

Kisha akatorokea kwenye nyasi kwa kasi.



Tangu siku hiyo, mamba angali anamngoja Buibui Anansi kwenye ukingo wa mto.

Pua na macho yake makubwa yanajitokeza juu ya maji.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Anansi, Kunguru na Mamba

Author - Ghanaian folktale
Translation - Mutugi Kamundi
Illustration - Wiehan de Jager
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org



Anansi na Kasa

Mutugi Kamundi
Wiehan de Jager

Kiswahili



Siku moja, Buibui Anansi, alivuna viazi vikuu shambani mwake.

Vilipendeza na kuonekana vitamu sana.

Alivichoma taratibu kwenye moto na akaanza kula.

Buibui Anansi alipokuwa akitia tonge la kwanza kinywani, mlango wake ulibishwa. "Lo! Lo! Lo!" alisema moyoni. "Huyo ni nani?"

Kasa, aliyeonekana mchovu, alisimama mlangoni. Kasa alisema, "Anansi, tafadhali niruhusu niingie. Nimetembea mwendo mrefu leo. Nimechoka na ninahisi njaa."

Buibui Anansi alimruhusu Kasa akaingia.

Buibui Anansi hakumgawia mwengine chakula chake kitamu, hata mgeni.

Kasa alipotaka kula, Buibui Anansi alimkemea, "Kasa, huwezi kula kwa mikono michafu. Nenda ukanawe kwanza."

Mikono ya Kasa kweli ilikuwa michafu sana kwani aliitembelea siku nzima. Kasa alijikokota hadi mtoni akanawa mikono kisha akarudi.

Buibui Anansi alibaki akibugia viazi kwa haraka. Kasa aliporejea hakupata kiazi hata kimoja.

Kasa alimwambia Buibui Anansi, "Asante kunialika kwa chakula cha jioni. Nami pia nitakukaribisha kwangu nikuandalie chakula kitamu."

Kasa alijikokota kuelekea nyumbani kwake.

Siku moja Buibui Anansi aliwasili nyumbani kwa Kasa kabla chakula cha jioni. Kasa alikuwa amejilaza chali akiota jua kama Kasa wafanyavyo.

Alipomwona Buibui Anansi, alisema, "Aa! Hujambo Anansi! Umekuja kushiriki nami chakula cha jioni?"

Buibui Anansi akaitikia, "Naam, nitafurahia sana, asante."

Anansi alikuwa akihisi njaa mno.



Kasa alipiga mbizi na kuzama chini ya mto akaandaa chakula cha jioni. Naye Buibui Anansi alingoja kando ya mto.

Baada ya maandalizi, Kasa alirudi juu ya maji akasema, "Kila kitu ki tayari, karibu. Twende tukafurahie mapochopocho."

Kasa alipiga mbizi tena na akaanza kula majani matamu aliyokuwa ameandaa.



Buibui Anansi alijaribu kujizamisha mtoni lakini, wapi! Yeye alikuwa buibui wala sio kasa. Alishindwa kupiga mbizi kabisa. Kila alipojaribu, alielea juu ya maji.

Alijaribu kuruka majini tena na tena lakini ng'o! Hakufanikiwa kukifikia chakula kilichoandaliwa na Kasa chini ya maji.

Hatimaye, Buibui Anansi alipata wazo zuri. Alitia mawe kwenye mifuko ya koti lake. Akawa mzito akaweza kuzama majini. Alikuwa mwerevu kwelikweli!

Sasa aliweza kuiona meza iliyojaa majani matamu na laini pamoja na vyakula vingine vya kupendeza. Alidondokwa na mate alipoviona vyakula hivyo.

Buibui Anansi alipokuwa akinyoosha mkono kuchukua chakula hicho cha kupendeza, Kasa alimkataza akisema, "Anansi, unawezaje kula ukiwa umevaa koti? Haiwezekani hapa kwangu."

Bila kufikiri, Buibui Anansi akasema, "Samahani! Bila shaka usemavyo ni kweli. Sikufikiria kuhusu hilo." Buibui Anansi, alilivua koti lake.

Punde tu alipolivua koti, Buibui Anansi alielea juu ya maji kwa sababu hakuwa na mawe ya kumwezesha kuzama.

Alihuzunika na akachopeka kichwa chake majini akawa anamtazama Kasa akila chakula hicho chote kitamu peke yake.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Anansi na Kasa

Author - Ghanaian folktale
Translation - Mutugi Kamundi
Illustration - Wiehan de Jager
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org

Anansi na Tai

Brigid Simiyu
Wiehan de Jager

Kiswahili

African Storybook.org



Buibui Anansi, na Sungura, walikuwa marafiki. Waliishi kwa amani kijijini milimani. Sungura alimiliki shamba kubwa lililojaa mboga na matunda.

Ingawa Sungura alimgawia rafikiye Anansi kwa ukarimu, Anansi hakufurahia na alimwonea wivu.

Buibui Anansi aliwaza jinsi angelinyakua shamba la Sungura na kulifanya kuwa lake. Alifaulu na kumwacha Sungura katika hali ya umaskini na bila makao.

Buibui Anansi sasa alijivunia kuwa mmiliki wa shamba lote la Sungura pamoja na mboga na matunda.

Siku moja, Buibui Anansi aliienda sokoni kuuza matunda na mboga. Alizipata hela nyingi akakijaza kikapu!

Alizitumia baadhi ya hela hizo kuinunulia familia yake nafaka. Aliweka nafaka hiyo juu ya hela zilizokuwa kikapuni.

Buibui Anansi alikibeba kikapu chake kichwani akaelekea nyumbani huku akiimba.

Wakati wote huo, alikuwa akiwaza juu ya vitu vyote ambavyo angetumia hela hizo zote kununa.

Alipokuwa njiani, kulikuwa na manyunyu ya mvua. Punde tu manyunyu yaligeuka na kuwa mvua kubwa iliyomwagika.

Buibui Anansi alikiacha kikapu chake pembeni mwa barabara naye akaenda chini ya mti kujikinga. Lakini alikichunga kikapu hicho cha thamani kutoka pale alikokuwa.

Mvua ilinyesha kwa wingi zaidi hadi Anansi akalowa na kuhisi baridi.

Aliamua kukimbilia shimoni. "Nitaketi hapa shimoni hadi mvua itakapoisha," alijiambia. "Bora hela zangu zimekingwa na nafaka niliyoweka juu yake."

Muda mfupi baadaye, Tai aliruka pahali pale na kukiona kikapu kando ya barabara. Aliona pia kwamba kulikuwa na fedha na nafaka.

Tai alikifunika kikapu hicho kwa mabawa yake na kusubiri mvua iishe.

Buibui Anansi alimwona Tai akiwa amekalia kikapu chake. "Ah asante rafiki yangu kwa kukilinda kikapu changu," alimwambia Tai.

"Samahani, Anansi, nilikusikia vyema?" Tai aliuliza. "Eti kikapu chako? Kikapu hiki ni changu! Nilikipata hapo pembeni mwa barabara!"

Buibui Anansi hakuweza kuamini masikio yake! "Ni changu, nakwambia!"

Buibui Anansi alienda kushtaki kwa Chifu. Tai aliwaambia Chifu na wazee, "Inawezekanaje kukiacha kikapu kilichojaa fedha na nafaka barabarani bila ulinzi wowote?"

"Nilikuwa nikikichunga kikapu changu. Fedha ni zangu na nafaka ni yangu!" Buibui Anansi alisema.

"Nilikuwa nimekikinga kikapu hiki kwa mabawa yangu ulipotokezea na kudai kwamba kilikuwa chako!" Tai alijibu.

Baada ya Chifu na wazee wake kusikiliza kwa makini pande zote mbili, waliwataka Buibui Anansi na Tai watoke hapo na kwenda mbali kidogo.

Walijadili kisa hicho kwa muda mrefu. Hatimaye, walifikia uamuzi.

Waliwaita tena Buibui Anansi na Tai. "Tunamwamini Tai," walisema. "Yeye si mwizi. Wewe Anansi, ulikuwa ukijitakia kitu kisichokuwa chako."

Buibui Anansi hakuweza kuamini masikio yake. Aliangua kilio.

Ujumbe ulisambaa kwamba uamuzi ulimwendea vibaya Buibui Anansi. Buibui Anansi alipoondoka, alimsikia Sungura akicheka kwa nguvu.

Sungura alirudi shambani kwake akaendelea kupanda matunda na mboga.

Buibui Anansi aliwapoteza marafiki wote. Alirejelea hali yake ya umaskini.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Anansi na Tai

Author - Ghanaian folktale
Translation - Brigid Simiyu
Illustration - Wiehan de Jager
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org



Demane na pacha wake

Mutugi Kamundi
Jemma Kahn

Kiswahili

ASb approved
African Storybook.org

Hapo zamani za kale paliondokea mvulana mmoja aliyeitwa Demane. Alikuwa na pacha mwenzake aliyeitwa Demazane.



Wazazi wao walipofariki, Demane na Demazane walienda kuishi na mjomba wao. Huko kwa mjomba wao, walitendewa mabaya. Walichapwa kwa vibiko virefu, na walipewa uji mwepesi mara moja tu kwa siku. Kwa sababu hiyo, walitoroka.



Hawakuwa na nyumba ya kuishi. Waliona pango wakaamua kuishi ndani mwake. Waliogopa kwa sababu walisikia kwamba majitu yaliyowala watu yaliishi karibu. Kwa hivyo waliunda mlango wenye nguvu. Wakafunga kiingilio na kuacha mashimo mawili ya kupitisha hewa na mwangaza. Kisha Demane akamwambia dadake, "Baki humu pangoni nikatafute chakula. Na usipike nyama kamwe. Majitu hupenda sana harufu ya nyama."



Kila jioni Demane alirudi na nyama ya sungura, ndege au paa. Kila aliporudi pangoni aliimba:

Demazane, Demazane,
nimefika kwenye pango,
nifungulie mlango,
ndiye mimi si uongo,
nimewinda na korongo,
tupike kwa kikaango,
ufungue kwa mpango,
asiingie muongo.



Kesho yake alipata ukakamavu, akawasha moto ili kuondoa baridi. Lakini aliwasha moto huo ndani ya pango kwa kuogopa majitu. Aliufunga mlango kabisa. "Nina hakika hakuna hatari nikichoma nyama kwa moto huu. Chakula cha kuchomwa ni kitamu."



Demane aliporudi nyumbani aliimba:

Demazane, Demazane,
nimefika kwenye pango,
nifungulie mlango,
ndiye mimi si uongo,
nimewinda na korongo,
tupike kwa kikaango,
ufungue kwa mpango,
asiingie muongo.

Demane aliingia na kuiona nyama. Aliuliza, "Uliichomaje nyama bila moto?" "Niliichoma kwenye jua nje ya pango," Demazane alijibu upesi. Demane alikuwa amechoka. Hakuuliza swali tena. Waliendelea kufurahia chakula.

Siku iliyofuata Demazane aliwasha moto akachoma nyama tena. Alpomaliza aliusikia wimbo.

Demazane, Demazane,
nimefika kwenye pango,
nifungulie mlango,
ndiye mimi si uongo,
nimewinda na korongo,
tupike kwa kikaango,
ufungue kwa mpango,
asiingie muongo.

Lakini sauti hiyo haikuwa kama ya kakake. Demazane akajibu, "Hapana, wewe si kakangu. Sauti hiyo si yake."



Baada ya muda mfupi alisikia sauti tena ikiimba:

Demazane, Demazane,
nimefika kwenye pango,
nifungulie mlango,
ndiye mimi si uongo,
nimewinda na korongo,
tupike kwa kikaango,
ufungue kwa mpango,
asiingie muongo.

Sauti hiyo ilifanana na ya kakake. Kwa hivyo aliufungua mlango.

Jitu kubwa lenye nywele mwili mzima lilijaa mlangoni. Likamchukua Demazane haraka. Lakini, Demazane aliokota jivu la jikoni akabeba. Alipokuwa akibebwa alimimina jivu lile njiani walikopitia.



Demane aliporudi alipata mlango ukiwa wazi na Demazane hakuwa ndani. Lakini aliona jivu lililomwagwa kulekea msituni. Alifuata jivu hilo mpaka alipoona moto mbali.





Demane aliona jitu lililojaa nywele limeketi karibu na moto. Mfuko mkubwa ulikuwa karibu naye. Alisongea karibu na jitu hilo akijifanya anachechemea kama mtu aliyeumia mguu. "Tafadhali babu," Demane alisema, "naomba unisaidie. Nimeumia mguu. Naomba maji ya kunywa." Jitu likasema, "Ngoja nikuletee maji lakini usiguse mfuko wangu. Jitu lilisema huku likiweka mfuko ule vizuri ndani ya nyumba."



Jitu lile lilipoondoka kwenda mtoni, Demane alikata kamba ya mfuko. Ulifunguka na dadake akatoka. Demane alibadilisha mfuko huo na mfuko wake uliojaa nyuki. Kisha yeye na dadake wakajificha na kungoja kuona kile ambacho kingetokea.



Jitu lilirudi na maji pamoja na watoto wake wawili, msichana na mvulana. Likamwambia msichana, "Kuna mlo mtamu ndani ya mfuko. Nenda ukaulete! Msichana alifungua mfuko kuona kilichokuwa ndani. Nyuki walimwuma mkono akalia akisema kwa sauti, "Inauma, inauma." "Nenda ukamsaidie," jitu lilimwambia mvulana kwa sauti. Pia mvulana aliumwa akalia kwa uchungu."



"Msinifanye mjinga," jitu lilisema kwa sauti likajitoma ndani ya nyumba. Lilifunga mlango na kufungua ule mfuko. Nyuki wale walichomoka kwa wingi na kumwuma kichwani, masikioni, na hata kwenye macho. Alishindwa kuona akarukaruka na kulia kwa uchungu mwingi.



Jitu lilikimbia kuelekea kwenye bwawa la maji. Lilichopeka kichwa kwenye matope likakwama huko. Liligeuka na kuwa kisiki cha mti uliokatwa. Nyuki walijenga mzinga wao kwenye kisiki hicho. Baadaye, Demane na Demazane walifurahia asali tamu kutoka kwa mzinga huo wa nyuki.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Demane na pacha wake

Author - South African Folktale
Adaptation - Mutugi Kamundi
Illustration - Jemma Kahn
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org

Familia ya Pembenyingi

Ursula Nafula
Isaac Okwir

African Storybook.org



"Mwaka huu tutakuwa na mkutano maalum wa familia," Mama Pembenyingi alitangaza. "Nani atakayehudhuria? Natumai Pembenyingi wote watakuwa. Ninawakosa binamu yangu," Kosi alisema. "Ninakosa zaidi upande wa familia yangu ya Pembenne," Mama alitabasamu. "Ndiyo, ni kitambo sana tangu tuwaone Mstatili, Mraba, na Msambamba," alisema Baba Pembenyingi. "Usisahau, wana watoto watatu sasa!" Mama alimkumbusha Baba.



"Na binamu wengine, je? Watakuja?" Fusi aliuliza. Mama alijibu, "Ndiyo, wao ni Pembenyingi, ingawa si Pembenne. Jina lao la ukoo ni Pembetatu. Watoto ni Pembetatu Pacha na Pembetatu Sawa." "Aa, ndiyo, familia ya Pembetatu!" alishangaa Fusi. "Lakini wanafanana sana na Pembenne." "La, sio kabisa," Mama alisema. "Pembetatu wana pande tatu, ilhali Pembenne wana pande nne, kama mimi."



Baba Pembenyingi aliongeza, "Nimefurahi kwa sababu binamu yangu wengine watatu watakuwa hapa, yaani, Pembetano, Pembesita na Pembenane. Wao pia ni wa familia yetu ya Pembenyingi." Vusi aliuliza, "Baba, mbona tunaitwa Pembenyingi?" "Tunaitwa Pembenyingi kwa sababu tuna pande mbili sura. Tumeumbwa kwa mistari iliyonyooka, na maumbo yetu yamefungika, kama unavyoona, mistari yetu yote imeunganika. Binamu yetu Pembetatu, Pembenne, Pembesita, na Pembetano wote watatutembelea," Baba alijibu.



"Je, ulisema kuwa Pembenane atakuja? Yeye pia ni jamaa yetu?" Khosi aliuliza. "Bila shaka, binti yangu, ukimtazama, utajua kwamba ni wa familia yetu. Unastahili kuangalia kwa makini idadi ya pande ambazo binamu yako wanazo, au hutaweza kuona tofauti. Binamu Pembenane ana pande nane kwa sababu jina lake linamalizika na nane," Baba alisema.



"Sawa, na Pembetano na Pembesita, je?" Vusi aliuliza. "Binamu Pembesita ana pande sita kwa sababu jina lake linamalizika na sita," Baba alijibu. "Pembetano wana pande tano. Mwalimu wetu alituambia kwamba tano inatokana na pande hizo tano," aliongeza Khosi. "Kumbuka kwamba tatu na nne ndizo zinafanya binamu yako Pembetatu na Pembenne kuwa tofauti.



"Baba, Pembesaba ana pande ngapi?" Vusi aliuliza. Baba alicheka akasema, "Sitakwambia. Kumbuka tulipiga picha zake tulipokuwa kwa harusi ya mjombako. Ningependa uitazame picha ile kwa makini kisha unieleze unachoona. Vusi aliitazama picha haraka halafu akajibu, Pembesaba ana pande saba!" Khosi aliongeza, "Ndiyo, kumbuka mwalimu wetu alituambia kuwa saba inatokana na idadi sab."



"Aa mke wangu, unaona jinsi watoto wetu walivyo werevu? Je, kumi ina maana gani?" Baba aliuliza. "Pembe kumi!" Vusi na Khosi walisema. "Ndiyo, hiyo ndiyo sababu binamu yenu anaitwa Pembekumi. Lakini, hatakuja kwa sababu ataiwakilisha timu ya waogeleaji. Kuna Pembekumi wachache sana shuleni kwao," Mama aliwaambia.



Watoto walisema, "Mama na Baba, tunaweza kumualika rafiki yetu Mduara?" Wazazi wao walikubali Mduara kujiunga nao kwa sherehe. Wakati huo, waliusikia mlango ukibishwa. Baba aliienda kujua ni nani. "Pembenne wako hapa! Karibu! Karibu!" Baba alishangilia.



Familia yote inaruka kuwasalimu Mraba, Mstatili, na watoto watatu wa Msambamba. Pembenne wanafurahi kuwa wa kwanza kufika.



Familia ya Pembetatu inabisha mlango muda mfupi baada ya kufika kwa Pembenne. Pembetatu pacha na Pembetatu sawa wamechoka baada ya safari ndefu. Lakini, wamefurahi kuwa pamoja na familia nzima.



Hatimaye, Pembenane na Pembesaba wanawasili pamoja na wanao, Pembetano na Pembesita. Pia wemewaleta Miraba watatu. Pembenane anaeleza, "Natumai si tatizo kwamba wana Pembenne watatu kutoka kijijini wamekuja nasi. Hawajawahi kwenda jijini." Mama alitabasamu, "Marafiki na familia wanakaribishwa hapa kila wakati." Aliwatuma watoto wote nje kucheza.



"Tutacheza mchezo gani?" Vusi aliwauliza watoto wengine. Pembetatu sawa alisema kwa furaha, "Hebu tucheze mchezo wa maumbo!" Watoto wote wa Pembenyingi walianza kucheza mchezo huo. "Ninaweza kucheza nanyi? Mimi pia ningependa kucheza mchezo wa maumbo," Mduara alisema. Vusi alimjibu, "Aibu kubwa, samahani, huwezi kucheza mchezo huo rafiki yangu." Mraba mmoja aliongeza, "Huoni umbo lako, wewe si wa familia ya Pembenyingi. Duara hawawezi kucheza mchezo wa maumbo."



Mduara alihuzunika sana kwa kuachwa nje ya mchezo. Lakini, mchezo haufurahishi sana mmoja akiachwa nje. Vusi alisema, "Ni heri tucheze mchezo ambao Mduara pia anaweza kucheza." Kwa hivyo, Pembenyingi na Mduara walicheza pamoja kwa furaha hadi chakula kitamu kilipokuwa tayari.



Your translated text



Your translated text



Your translated text

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Familia ya Pembenyingi

Author - Lindiwe Tshabalala and African Storybook
Translation - Ursula Nafula
Illustration - Isaac Okwir
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2016
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org

Hakimu asiyekuwa na busara

Ursula Nafula

Brian Wambi

Kiswahili

African Storybook.org

Hapo zamani, waliishi majirani wawili marafiki, Meseret na Demeke. Walikuwa maskini sana.

Siku moja, Meseret alimwambia Demeke, "Lazima leo niipeleke ngano yangu sokoni. Gunia ni nzito na soko iko mbali. Ningekuwa na pesa za kutosha, ningemnunua punda."

Demeke alijibu, "Nami lazima nikavinunue vyungu vipya leo sokoni. Vitakuwa vizito mno. Heri ningekuwa na punda vilevile. Kwa sasa, ninazo tu nusu ya pesa."

Meseret alikuwa na wazo. Alisema, "Hebu tumnunue punda pamoja. Wewe utalipa nusu nami nilipe nusu. Nitamtumia kwenda sokoni kwa juma moja nawe umtumie kwa juma lingine."

Meseret na Demeke walimnunua punda. Kwa muda mrefu waliishi kwa furaha.

Siku moja, babake Meseret alifariki. Meseret alirithi mashamba, miti, ng'ombe na kondoo.

Alikuwa tajiri na hakutaka kufanya kazi na Demeke tena. Vilevile, alitaka nusu yake ya punda.

Meseret alimwambia Demeke, "Mbwa wangu wanahitaji nyama. Ninataka kumchinja punda wetu wewe uchukuwe nusu yake nami nichukuwe nusu itakayobaki."

Demeke alilia, "Sihitaji nyama yoyote ila punda. Ikiwa unataka kumchinja, nipe pesa za nusu yangu." Meseret alifoka, "Sitakupatia pesa zozote. Nusu ya punda ni yangu na ninaitaka sasa." Demeke alisema, "Hebu twende kwa hakimu atuamulie."

Meseret na Demeke walienda kumwona hakimu alisiyekuwa na busara. Hakuwasikiliza kwa makini.

Hakimu aliwauliza, "Mnammiliki punda pamoja?" "Ndiyo," Meseret na Demeke waliitikia. Hakimu akasema, "Basi, kila mmoja atapata nusu. Iwapo Meseret anataka nusu yake, ana haki ya kuichukuwa. Mchinjeni punda kisha mmgawe nusu mbili."

Meseret alifurahi. Alimchinja punda na kuchukua nusu ya nyama kuwapelekea mbwa wake.

Demeke alihuzunika akawaza, "Maskini punda wangu hayupo tena, na sasa lazima nibebe kila
kitu mwenyewe."

Baadaye, Meseret alitaka kujijengea nyumba mpya. Alifikiri, "Nitakiteketeza chumba changu kizee kisha niijenge nyumba mpya nzuri na kubwa." Meseret alivihamisha vitu kutoka chumbani.

Demeke alimwuliza, "Unafanya nini?" Meseret alimjibu, "Ninataka kukiteketeza chumba changu ili niijenge nyumba mpya."

Demeke alikuwa na wasiwasi, "Lakini, chumba chako ki karibu na changu. Ukikiteketeza, changu pia kitateketea."

Kwa hasira, Meseret alisema, "Usijaribu kunizuia! Hiki ni chumba changu na nikitaka nitakiteketeza." Demeke alilia, "Wacha! Hebu twende tumwulize hakimu."

Kwa sababu hakimu hakuwa mwenye busara, hakusikiliza kwa makini wala hakuelewa. Hatimaye alisema, "Meseret ana haki ya kukiteketeze chumba chake na hakuna anayeweza kumzuia."

Meseret alipokiteketeza chumba chake, upepo uliupeperusha moto hadi kwenye paa la chumba cha Demeke. Punde, chumba chake pia kilianza kuteketea.

Demeke alimlilia hakimu, "Tazama! Meseret amekiteketeza chumba changu! Lazima anilipe." Hakimu aliamua, "La! Meseret alikiteketeza chumba chake. Moto ndio uliokiunguza chumba chako. Meseret hastahili kukulipa."

Maskini Demeke alihuzunika sana. Hakuwa na punda wala chumba. Alibaki na shamba peke yake.

Kila siku alifanya kazi shambani mwake na usiku kulala chini ya mti.

Demeke alifanya kazi kwa bidii shambani mwake. Aliyang'oa magugu na kuwafukuza ndege.

Wakati wa kuvuna ulipofika, kulikuwa na mazao mazuri ya mbaazi.

Siku moja, wanawe Meseret walipitia katika shamba la Demeke.

Waliona mbaazi wakasema, "Mbaazi ni tamu sana!" Walizivamia wakazitoa zote.

Demeke alipowaona wanawe Meseret, aliwaambia, "Nirudishieni mbaazi zangu."

Walimjibu kwa dharau, "Hatuwezi kukurudishia kwa kuwa tumezila. Mwulize baba akulipe."

Demeke alimwambia Meseret, "Wanao wamezila mbaazi zangu." Meseret alimjibu, "Nitakupa pesa."

"Sitaki pesa zako. Ninataka mbaazi zangu." Demeke alitishia.

"Subiri! Hebu twende tumuulize hakimu," Meseret alilia.

Meseret na Demeke walimwona hakimu yule yule. Kama kawaida, hakuwasikiliza kwa makini wala hakufikiria juu ya tukio hilo. "Wanawe Meseret walikula mbaazi zako na ni lazima zirudishwe. Pasua tumbo zao uchukuwe mbaazi zako." Hakimu aliamua.

Meseret alisononeka sana akasema, "Wanangu watafariki! Tafadhali, Demeke, nitakupatia pesa." "Nilitaka pesa ulipomchinja punda wetu. Ninataka mbaazi zangu." Demeke alinena.

Demeke alichukua kisu chake. "Nitakujengea chumba kipya! Naomba msamaha kwa kukiteketeza chumba chako cha kwanza," Meseret alisema.

"Sitaki chumba kipya. Ninataka mbaazi zangu," Demeke alimjibu. Alianza kukitia kisu chake makali. "La! La! Tafadhali, ngoja! Hebu twende tukawaone wazee. Tafadhali rafiki yangu wa jadi, wacha wazee waamue." Meseret alilia.

Meseret na Demeke walienda kuwaona wazee wa kijiji. Wazee waliongea kwa muda mrefu.

Mwishowe walimwambia Meseret, "Ulikosea ulipokataa kumlipa Demeke nusu ya punda wake. Ulikosea pia ulipokiteketeza chumba chake, na wanao walipozila mbaazi zake."

Wazee walimgeukia Demeke wakasema, "Unataka kuwaua wanawe Meseret. Hilo ni kosa pia. Huu ni uamuzi wetu. Lazima Meseret ampatie Demeke nusu ya miti yake yote, mashamba, ng'ombe na kondoo. Hivyo, mtaishi pamoja kwa amani."

Meseret alimpatia Demeke nusu ya mali yake.

Waliishi pamoja kwa furaha bila kugombana tena.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Hakimu asiyekuwa na busara

Author - Magabi Eynew Gessesse and Elizabeth Laird
Translation - Ursula Nafula
Illustration - Brian Wambi
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2016
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org
Original source www.ethiopianfolktales.com



Jambazi

Susan Kavaya
Jacob Kono

Kiswahili

African Storybook.org



Hapo zamani za kale, kulikuwa na wafanya biashara waliokwenda kila mahali. Walisafiri wakati wa musimu wa baridi na musimu wa joto.

Walivuka milima, majangwa na misitu wakiuza na kununua bidhaa.

Wafanya biashara hao waliwaogopa majambazi, kwa hivyo walisafiri wakiwa katika vikundi.

Ilitokea kuwa mfanya biashara mmoja hakuweza kupata kikundi cha kusafiri nacho, kwa hivyo, alisafiri peke yake. Alikutana na jambazi akajawa na hofu.

Jambazi huyo alimwuliza, "Wewe ni nani?"

Alijibu, "Mimi ni mfanya biashara."

"Uko peke yako?"

"La! Marafiki zangu wako nyuma ingawa sasa niko peke yangu." Alijibu.

Wakati huo, mfanya biashara mwingine alikuja kutoka nyuma yao. Alijificha akatazama kwa hofu jambazi yule akimwua mfanya biashara wa kwanza na kumzika.

Aliwaza, "Nitaendeleaje na safari yangu? Yaliyompata mwenzangu yatanipata mimi pia." Aliogopa kuvuka akabaki mahali hapo kwa muda.

Baadaye, aliwaza, "Siwezi kukaa hapa milele. Lazima niendelee na safari yangu."

Alipita mahali ambapo jambazi alikuwa amemwua mfanya biashara wa kwanza. Alifika kijijini akiwa amehuzunika sana. Hakuweza kutabasamu wala kuzungumza na watu.

Watu walimwuliza, "Ulikuwa mchangamfu, lakini sasa umehuzunika. Kwa nini?"

"Nimechoka na ninahisi kiu," alisema.

Alikaa hapo kijijini usiku wote. Siku iliyofuata, aliendelea na safari yake.

Watu walizidi kumwuliza, "Unasumbuliwa na nini?"

Mfanya biashara alijiuliza, "Je, niwaambie au la?" Mwishowe, aliamua kuwaambia yaliyompata mfanya biashara mwenzake.



Alipomaliza kuwasimulia, wanakijiji walijua kuwa jambazi alikuwa ametoka kijijini kwao.

Walisema, "Ni vibaya sana kitendo kama hiki kutendeka hapa. Tutajaribu kujua aliyeuawa ni nani."

Lakini, hawakusema jambo lolote kuhusu jambazi aliyemwua mfanya biashara huyo.

Mfanya biashara yule aliwaambia wanakijiji, "Nilimuona mtu akizika maiti ya mtu mwengine. Sikujua aliyezikwa alikuwa nani wala jambazi alikuwa nani. Sitawahi kurudi mahali hapa tena."

Mfalme wa kijiji alisikia jinsi wafanya biashara walikuwa wakiuawa na kuzikwa na majambazi.

Alihuzunika. "Je, majambazi wanawezaje kuwafanyia wafanya biashara hivi katika milki yangu?"

Alitafuta njia ya kusuluhisha tatizo hilo. "Nitawaalika watu wote katika sherehe kisha nijaribu kuwashika majambazi hao."

Mfalme alipendwa sana na watu wake. Aliwaandalia sherehe wakulima, makasisi na kila mtu kijijini. Wote walikula, wakanywa na kujiburudisha.

Mfalme akasema, "Binti yangu ni mgonjwa. Dawa pekee inayoweza kumponya ni ndimu inayomea karibu na maji yaliyo baridi mbali na wanapoishi binadamu. Kuna yeyote anayeweza kuniletea ndimu hiyo?"



Kila mtu aliwaza, "Je, nitaipata wapi ndimu aina hiyo?"

Hawakusema chochote ila jambazi alisimama haraka akasema, "Mheshimiwa, nitakuletea ndimu hiyo, lakini nipe muda wa wiki mbili."

Jambazi alikwenda moja kwa moja mpaka mahali alipomzika mfanya biashara aliyemwua kwa sababu ndimu aliyotaka mfalme ilimea hapo.

Alikimbilia kuipata kabla mtu mwingine kufanya hivyo. Aliziweka ndimu mfukoni halafu akakimbia kumpelekea mfalme.

Baada ya kusubiri langoni kwa siku kadhaa, alikubaliwa kumwona mfalme.

Alisema, "Niko tayari kutimiza mahitaji yako. Nimekuletea ulichokitaka. Tafadhali kipokee."

Mfalme alisema, "Nimefurahi umekileta nilichotaka. Ningependa unipe tukiwa mbele ya watu wengi."

Mfalme aliwaita watu wote kutoka kijijini kwenda katika ikulu.

Walipokuwa wanakula na kunywa, alisema, "Mtu huyu ametimiza ahadi yake kama mlivyosikia. Alisema ataleta tunda nililohitaji na amelileta. Ningependa kupokea zawadi hii kubwa mbele yenu nyote."

Watu walifikiri kuwa jambazi angepata zawadi ya pesa. Walimwonea wivu. Walishangaa jinsi alipata matunda hayo ya pekee.

Jambazi aliufungua mfuko wake ili kumpatia mfalme ndimu mbili.

Alipozitoa mfukoni, zilikuwa ndimu mbili, lakini alipomkabidhi mfalme, zaligeuka na kuwa mafuvu mawili ya binadamu.

Hili lilipofanyika, watu wote walikasirika, naye jambazi akapigwa na butwaa.

Mfalme alitabasamu.

Kwa muda mrefu, alikuwa akitamani kukomesha ujambazi katika ufalme wake. Alitaka vitendo vyao viovu kujulikana kwa kila mtu. Alikuwa akiomba Mola amwonyeshe nani aliyekuwa jambazi.

Siku hiyo, maombi yake yalijibiwa.

Alijua mtu huyo ndiye aliyekuwa muuaji.

Alitoa amri atiwe gerezani.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Jambazi

Author - DiresGebre-Meskel and Elizabeth Laird
Translation - Susan Kavaya
Illustration - Jacob Kono
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2016
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org
Original source www.ethiopianfolktales.com

Kumsubiri mtoto

Ursula Nafula
Catherine Groenewald

Kiswahili

African Storybook.org

Leo ni siku kubwa! Baada ya kusubiri kwa miezi 9, mamake Taby anaenda hospitalini kujifungua mtoto. Atarudi baada ya siku tatu.

Unaweza kusoma tarehe na siku hiyo kwenye kalenda? Itakuwa tarehe gani mamake Taby atakaporudi nyumbani?

"Kwaheri mpendwa!" Mamake Taby anasema. "Tafadhali, msaidie babako. Nitarudi nyumbani hivi karibuni nikiwa na zawadi itakayotushangaza sote!"

Mtoto aliye tumboni kwa mama amekua mkubwa sana. Taby hawezi kumkumbatia mamake kama ilivyokuwa hapo mbeleni.

Dereva wa teksi anapiga honi. Wakati umefika wa mama kuondoka. Taby anaanza kulia. Babake anambeba mabegani kwake. Taby hupenda kuwa juu kama alivyo sasa. Sasa yeye ni mrefu kumliko babake.

Ikiwa urefu wa babake Taby ni sentimita 160, je, sasa Taby yuko umbali gani kutoka chini?

Muda mfupi baadaye, Taby anaanza kulia tena. Hii itakuwa mara ya kwanza kabisa kwa Taby na mamake kutengana.

Babake Taby anamweka kwenye kiti kilicho mbele yake. Anamfuta machozi kisha anamzungumzia polepole kumfariji.



Anapokuwa amesimama kwenye kiti, Taby anafurahi tena. "Nina umri wa miaka 6! Mimi sasa ni msichana mkubwa!" Taby anasema. Anaposimama kitini kama alivyo sasa, Taby anakuwa mrefu kama babake alivyo.

Je, unakumbuka urefu wa babake? Je, Taby ni mrefu kiasi gani anaposimama sakafuni?

Taby atasubiri tu siku tatu kuanzia Jumatano hadi Jamamosi, lakini kwake ni kama miaka. Anajaribu kuhesabu saa ambazo atalazimika kusubiri.

Anajua kuwa kuna saa 24 kwa siku, kwa hivyo anajiambia, "24 + 24 + 24 ni_____."

Unajua jawabu?

Taby anasema, "Baba, nilidhani kwamba mimi ni mtoto wako! Hivyo ndivyo unavyoniita. Itakuwaje sasa? Je, nitakoma kuwa mtoto wako?"

Babake anamwambia, "Wewe ni mtoto wetu wa kwanza wa pekee. Na hivyo ndivyo utakuwa wakati wote."

Baba anajibu maswali mengi kuhusu mtoto mpya. Kisha anapata wazao. "Mbona usimwandikie mama barua? Unaweza kumwelezea vile unavyomkosa na kumwuliza maswali kuhusu mtoto atakayezaliwa."

"Ningependa sana kufanya hivyo, baba. Utanisaidia kuandika?" Taby anamwambia babake.



Baada ya chakula cha mchana, baba anamsaidia Taby kumwandikia mamake barua. Isome barua aliyoiandika Taby:

Kwa Mama, Ninakupenda na ninakukosa sana! Baba anasema kuwa utarudi nyumbani Jumamosi. Nina hamu ya kukuona wewe na mtoto. Nina maswali mengi sana. Mtoto wetu mpya ni mvulana au msichana? Atanifanana? Je, ataanza lini kutembea au kuzungumza?

Upendo kutoka kwa Taby, binti yako mkubwa.

Anapomaliza kuandika barua yake, Taby anaanza kuota.

Kisha anafikiri, "Labda watakuwa watoto wawili. Labda, watakuwa mapacha kama baadhi ya marafiki zangu." Taby anafikiria juu ya Zubeda na Brenda, dada mapacha wanaofanana kabisa.

"Mapacha wetu wanaweza kuwa wa aina gani?" anaendelea kuwaza.

Siku iliyosubiriwa kwa hamu, inafika na Taby anasisimkwa sana. Alikuwa amesubiri kwa siku tatu, au saa 72, lakini ilikuwa kama miezi mingi tangu mamake alipoenda hospitalini.

Wamesubiri miezi 9 kwa mtoto kua tumboni mwa mamake. Taby anahesabu miezi kurudi nyuma, "Aprili mpaka Machi, ni mwezi 1, hadi Februari ni miezi..."

Hesabu kurudi nyuma ili upate mwezi hasa mtoto alipoanza kua tomboni mwa mama.

Taby anawasikia wazazi wake wakiwa mlangoni. Anakimya akitaka kuwashangaza.

Lakini, yeye ndiye anayeshangazwa. Mamake alikuwa amekuja nyumbani na mapacha! Taby sasa amepata dada na ndugu!

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Kumsubiri mtoto

Author - Ursula Nafula
Translation - Ursula Nafula
Illustration - Catherine Groenewald
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org

ASb approved

Mamba aliye mwilini mwangu

Ursula Nafula
Felicity Bell

Kiswahili

African Storybook.org

Ninaitwa Molly. Mimi ni msichana kama wasichana wangine, isipokuwa, nina mamba mwilini mwangu. Wewe huwezi kumwona, lakini ninajua yupo.

Jina lake ni Ukosefu-Kinga-Mwilini. Anajificha ndani ya mwili wangu na hawezi kuwaumiza marafiki zangu.

Mamba huyu hawezi kuondoka mwilini mwangu na kuingia mwilini mwako.

Hata ukikaa karibu nami au ukiushika mkono wangu.

Hawezi kuuacha mwili wangu na kuruka ndani ya wako ukila nami chakula cha mchana.

Au, hata ukilala karibu nami sakafuni.



Mamba huyu, Ukosefu-Kinga-Mwilini, amekuwa nami tangu nizaliwe.

Anapenda kuwala majeshi wote wa mwilini ambao wangepigana na viini na kunizuia kuwa mgonjwa.

Anapowala majeshi wangu kwa wingi, ninaugua sana. Siwezi kwenda shule wala kucheza na marafiki zangu.

Ninalazimika kumeza dawa zangu kila siku wakati unaopendekezwa. Nisipofanya hivyo, mamba huyu anaamka kwa hasira na kuwala majeshi wangu tena.

Mimi sitaki afanye hivyo. Ndiyo sababu ninamkumbusha bibi kunipa dawa zangu wakati unaofaa.

Nikila mboga na matunda, majeshi walio mwilini mwangu wanapata nguvu. Mamba huyu hawezi kuwashika.

Anapolala kwa muda, mimi huwa na nguvu. Hufurahi na kucheza na marafiki zangu tena.



Bibi alinipeleka kituo cha afya muda mfupi uliopita. Alipewa dawa na daktari ya kumfanya mamba huyu alale asiweze kuwala majeshi wangu.

Mimi huweza kukimbia, kupanda juu na kucheza kama watoto wengine.

Ninampenda bibi sana. Ni mzuri na mwenye huruma. Ananilisha chakula kizuri na kuhakikisha ninapata vitamini zaidi ili majeshi wangu wawe na nguvu.

Nikiugua, ananipeleka kituo cha afya mara moja ili nipate matibabu na kupata nafuu.

Ninafurahi anaponisomea hadithi kabla mimi kwenda kulala. Kabla sijalala, mimi huwaza juu ya kusomea katika shule kubwa.



Nitaendelea kuzitumia dawa za kumfanya mamba wangu alale. Ningependa kumsaidia bibi na kumsomea hadithi atakapozeeka na kutoweza kuona vizuri.

Nikiwa mtu mzima, ningependa kusoma na kuchangia kutafuta dawa zitakazowafanya mamba wote walio katika miili ya watu, walale milele daima.

Nitajifunza kuishi na mamba wangu na kufanya alale zaidi nitakavyoweza.

Nitakuwa na marafiki wengi na kufurahi kila siku iwezekanavyo.

Bibi, shangazi, wajomba, na marafiki, wananipenda, ingawa nina mamba mwilini mwangu anayeitwa Ukosefu-Kinga-Mwilini.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Mamba aliye mwilini mwangu

Author - Val Morris
Translation - Ursula Nafula
Illustration - Felicity Bell
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© Books In Homes 2013
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org

Matunda

Translators without Borders

Wiehan de Jager

Kiswahili

Hapo zamani, familia moja ilikuwa na mti wa matunda matamu yaliyowavutia wengi kutaka kuyaonja.

Familia hiyo pia ilikuwa na binti mzuri mrembo. Urembo wake na tabia zake nzuri vilisifiwa na watu wengi.

Alipokua mtu mzima, wanaume, vijana kwa wazee, walienda kwao wakiwa na nia ya kumposa.

Wazazi wa yule msichana walifanya uamuzi. Mwanamume ambaye angeketi pale nyumbani siku nzima bila kula tunda lolote, angeozwa binti wao.

Habari hiyo ilisambaa kijiji kizima. Mtu wa kwanza kufika alikuwa kiongozi wa wakulima wote kijijini.

Alikuwa tajiri mwenye sura nzuri tena alikuwa angali kijana. Alikaribishwa akaandaliwa matunda.

Lakini, kabla ya muda kupita, aliyala matunda kisha akaagwa akaenda zake.



Aliyefuata alikuwa kiongozi wa wafugaji. Yeye pia alikuwa tajiri mwenye sura nzuri na alikuwa angali kijana.

Msichana alipendezwa naye. Lakini alipoandaliwa matunda, aliyala mara moja.

Yeye pia aliagwa akaenda zake.

Wa tatu alikuwa na mashamba mengi, lakini, jeuri na mwenye sura mbaya. Msichana aliomba Mungu yule mtu ale matunda upesi ili aweze kwenda zake.

Alipoandaliwa matunda, alikataa kula. Wakati ulipopita, msichana alimwomba ale. Ilipofika saa kumi, alizidiwa na njaa akala.

Yeye pia aliagwa akaenda zake.

Aliyefuata, alikuwa mzee mwenye sura mbaya, mlaji rushwa asiyekuwa na adabu. Hakupendwa na yeyote kijijini. Msichana alitumaini angekula moja kwa moja na kwenda zake.

Alipoandaliwa matunda alikataa kula. Ilipofika saa kumi na mbili ya jioni, aliomba kwenda haja. Aliporudi, alinukia matunda huku midomo yake ikiwa na rangi nyekundu!

Msichana alifarijika mzee alipoagwa na kwenda zake.

Siku chache zilipita kisha mwana wa mfalme, aliyekuwa kijana, tajiri na mwenye sura ya kupendeza, alifika.

Msichana alimtazama akapendezwa naye mno. Msichana alimpeleka faraghani akamwomba asile matunda. Alimwandalia matunda machache kuliko waliyoandaliwa waliomtangulia.

Ilipofika adhuhuri, alikuwa amekwisha kula akaagwa. Msichana masikini alilia machozi ya hasira na hasara.

Siku iliyofuata, mkulima masikini na mvivu alifika pale. Alikuwa mwenye sifa ya kubobea maneno ambayo yaliwafurahisha watu. Akafika akiwa na nia madhubuti kushinda.

Msichana naye alimwandalia matunda mengi akamwomba ale aende zake. Alikataa kula. Msichana alisubiri kwa hofu.

Saa sita alikuwa hajala. Ilipofika saa kumi, aliomba maji.

Msichana alimwomba Mungu ale, lakini hilo halikutendeka.

Wazazi wa yule msichana hawakuwa na budi ila kumkubali "yule mvivu." Msichana naye alitamani kunusurika na mtu yule, lakini wazazi hawakuweza kumsaidia.

Walipokuwa njiani kwenda kwao nyumbani, mkulima alipiga makofi akiimba wimbo mzuri ambao uliwavutia watu waliokuwa barabarani.

Miongoni mwa watu wale walikuwa watumishi wa mwana mfalme. Walimwita mkulima wakamhonga kwa pesa pamoja na ng'ombe mradi akubali kumwacha msichana.

Bila kusita, akakubali pesa pamoja na ng'ombe akaenda zake peke yake.

Watumishi wale walimvisha msichana libasi murua mno wakampeleka mpaka jumba kubwa la mfalme.

Muda si mrefu, wazazi wake waliitwa na harusi ikaandaliwa.

Niliwaacha wakisherehekea nami nikaja kuwahadithieni ninyi.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Matunda

Author - Shakira Bodio
Translation - Translators without Borders
Illustration - Wiehan de Jager
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org

Mbweha na Jua

Brigid Simiyu
Manyeka Arts Trust

Kiswahili



Hapo zamani, palikuwa na Mbweha.

Alikuwa mvivu pia mjinga.

Yeye na babake mzee waliishi jangwani Kalahari.

Asubuhi moja, Mbweha mzee aliamka na kumpata mwanawe amelala juani.

Kifungua kinywa hakikuwa tayari na mbuzi walikuwa bado zizini!

"Wewe kijana mvivu sana! Nenda ukamtafute mke. Nimezeeka na siwezi kukukimu tena," babake alisema.

Mbweha kijana aliruka juu na kuwapeleka mbuzi malishoni.



Kichakani, aliona kitu kilichoangaza juu ya mwamba.

Alipoukaribia mwamba ndipo mwangaza ulipozidi kupendeza.

Labda huyu ndiye aliyekuwa mke wake!



"Wewe ni mzuri mno," Mbweha kijana aliueleza mng'aro. "Lakini, wewe ni nani? Mbona uko peke yako?"

"Mimi ni Jua," mng'aro ulijibu. "Familia yangu iliniacha hapa ilipohama. Haikutaka kunibeba maanake mimi ni moto sana."



Mbweha alisema, "Lakini, wewe u mzuri sana! Mimi nitakubeba. Nitakupeleka nyumbani nikujulishe kwa babangu."

"Ni sawa, unaweza kunibeba, lakini, usilalamike nikizidi kutoa joto usiloweza kuhimili," Jua lilisema.



Mbweha kijana alienda nyumbani bila ngozi, manyoya mgongoni, wala mke.



Babake Mbweha aliuuguza mgongo wa mwanawe kwa kutumia mafuta.



Polepole, manyoya yaliota tena.



Manyoya hayo mapya yalikuwa rangi tofauti na yale aliyozaliwa nayo.

Rangi hizo tofauti zilimkumbusha Mbweha kila mara kutokuwa mjinga tena.

Maelezo kuhusu hadithi:

Katika mwaka wa 2005, mwanahadithi wa Naro kwa jina la Bega Cgaze kutoka Jangwa la Kalahari nchini Botswana alimsimulia Marlene Winberg hadithi hii ambaye anaielezea hapa. Hadithi inapatikana katika mitindo tofauti katika jamii nyingi za kiSan za Afrika ya Kusini. Inawaonya vijana wengi wa kiume dhidi ya kudanganywa na urembo wa kimwili wa wasichana, na inawaelezea wazazi kutowalazimisha watoto wao kuoa kwa ajili ya kupata msaada wa nyumbani. Vilevile inaonyesha nguvu za jua jangwani. Michoro imefanywa na Marlene na kufafanuliwa na Satsiri Winberg kupitia weledi wa kikundi cha Manyeka cha Kisanaa.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Mbweha na Jua

Author - Traditional San story
Translation - Brigid Simiyu
Illustration - Manyeka Arts Trust
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© Manyeka Arts Trust 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org
Original source www.manyeka.co.za

ASb approved

Mti ulionusuru kijiji cha Balantu

Mutugi Kamundi
Julia te Water Naude

Kiswahili

African Storybook.org

"Shhhu!" Bibi alisema. "Kuna joto kali. Na chungu hiki ni kizito sana. Hebu tupumzike kidogo chini ya kivuli cha mti." Alijipangusa jasho usoni huku akiegemea mizizi ya mti.

Sela naye alisimama huku ameushika huo mbuyu kwa mkono mmoja. Nduguye, Tovo, aliuzungukazunguka ule mbuyu akiangalia ukubwa wake.

"Bibi, mbuyu huu ni mzee sana, sivyo?" "Ndiyo, Sela. Lakini sio mzee au mkubwa zaidi ya mbuyu ulio katika kijiji cha Balantu!" "Balantu? Kijiji hicho ki karibu?" Sela aliuliza. "Tafadhali tueleze kuhusu mti huo," Tovo alisema.

"Basi ketini msikilize," Bibi alisema huku akianza kuwahadithia.

Katika kijiji cha Balantu kuliishi msichana aliyeitwa Hami. Siku moja, Hami na ndugu yake Angula, walienda kuchota maji.

Hami alipokuwa akijaza chungu chake, Angula alimwona sungura. Alimkimbiza, lakini hakuweza kumshika.

Sungura alikuwa na mbio kumshinda.

Chungu cha Hami kilijaa maji. Sasa alikuwa tayari kwenda nyumbani. Aliangalia kila upande akamkosa Angula. Hakujua alikokwenda. Aljiua kwamba hangeenda nyumbani bila nduguye mdogo.

Alitazama kila mahali lakini hakumwona. Alipomtafuta, alimpata akiwa amelala kwenye nyasi nyuma ya kichuguu kikubwa.

Alipokuwa anamkaribia, Angula alimwashiria kwamba anyamaze. Mbona anyamaze?



Karibu na pale kulikuwa na kundi la vijana. Walikuwa wamebeba mishale, nyuta na mikuki! Hami aliweza kusikia sauti zao.

"Angula," Hami alimwita kwa sauti ya chini. "Wanaume hao ni wezi wa mifugo. Wamekuja kuiba ng'ombe wetu na kuchoma nyumba zetu. Njoo haraka. Lazima tukimbie nyumbani tukawatahadharishe wanakijiji."

Basi waliondoka polepole kutoka eneo hilo kisha wakakimbia kwenda nyumbani.

Hami alimwita mjomba kwa sauti, "Mjomba, kimbia, kimbia! Kuna wanaume wamekuja kuiba ng'ombe na kuteketeza nyumba." Mjomba alimrudisha ng'ombe kijijini.

Hami alimwita shangazi, "Shangazi, kimbia, kimbia!" Wanume wanakuja kuiba ng'ombe wetu na kuteketeza nyumba zetu!" Shangazi alichukua jembe lake, akambeba mtoto aliyekuwa akilala kisha akurudi kijijini.

Hami akamwona babu yake akiwa na punda wake. Akamwita kwa sauti, "Babu, kimbia, kimbia, wanaume wanakuja kuiba ng'ombe wetu na kuteketeza nyumba zetu."

Babu alimpiga punda akaenda mbio kuelekea kijijini.

Hami na nduguye wakafika kijijini. Hami akawaita watu wote kwa sauti, "Kimbieni, kimbieni. Kuna wanaume wanaokuja kuiba ng'ombe wetu na kuteketeza nyumba zetu!"

Wanakijiji wakawa na hofu sana. Wakawa wamechanganyikiwa kama kundi la mchwa lililokanyagwa na ng'ombe. Hawakujua pa kujificha wala la kufanya.

Wangewaficha ng'ombe wao wapi? Wangezificha nafaka zao wapi?

Wangejificha wapi wao wenyewe?

Hami aliogopa sana.

Akakumbuka mahali ambapo yeye na Angula walikuwa wakienda kucheza wakati mwingine.

Mahali salama.

Mahali pa siri.

"Ninapajua mahali ambapo sote tunaweza kujificha!" Lakini wanakijiji hawakumsikiliza. Walikuwa wakipiga kelele sana.

Sasa angefanyaje ili wamsikilize? Unadhani Hami alifanya nini?

Alichukua ngoma na kuipiga kwa nguvu kabisa. Bam! Bam! Bam! Boom! Boom! Boom!

Wanakijiji wote walitulia. Hami akawaambia kwa sauti, "Ninajua mahali ambako tunaweza kujificha. Nifuateni."

Hami alimshika Angula mkono akasema, "Njoo tawapeleke wanakijiji kwenye mti wetu. Sote tutakuwa salama huko."

Angula alitikisa kichwa. "Hapana, Hami. Mahali hapo ni siri yetu. Ulisema tusimwambie mtu yeyote."

"Ndiyo", Hami akasema. "Ilikuwa siri yetu. Lakini sasa sote tuko hatarini."

Hami na Angula waliwaongoza wanakijiji. "Kwa nini unatuleta hapa? Hatuwezi kujificha hapa," walisema.

Hami akamwita babake, "Nitakuonyesha." Hami na babake waliingia wakashuka ndani kupitia shimo dogo. Pale chini kulikuwa na uwazi mkubwa. "Lakini watu wote hawawezi kuingilia kwenye shimo dogo pale juu," babake alisema.

"Hapana," Hami alisema. "Tutaleta shoka tutengenze mlango wa kuingilia hapa kwenye shina."

Walitengeneza kiingilio shinani. Wanakijiji wakaleta vyakula na vyombo vya kupikia. Wote wakaingia ndani ya uwazi mkubwa wa mbuyu. La kushangaza ni kwamba kulikuwa na nafasi ya kuwatosha wote.

Wakati jua lilipotua na giza kutanda, kijiji kizima kilitulia tuli! Ulikuwa usiku wenye baridi.

Wale wahalifu walitembea taratibu kuelekea kijijini.
"Lazima wanakijiji wawe wamelala sasa," waliambiana.

Nao wanakijiji walijificha ndani ya mti. Nini kingetokea? Walihisi baridi na woga.

Hami akasema, "Kuna baridi sana. Tuwashe moto." Akachukua mawe mawili akayachua, moja juu ya jingine haraka haraka.



Baada ya muda mfupi, cheche za moto zikashika nyasi.

Kisha moto mkubwa ukawaka wakaanza kuota.



Nje, wavamizi walizidi kukaribia. Ghafla, mmoja wao alipiga mayowe akionyesha mbuyu walimojificha. Ndimi za moto zilitoka mle. Macho makali yaliangaza kutoka mle. Moshi ulipaa angani.

"Ni jinamizi kubwa!" Walilia kwa woga. Kwanza mvamizi mmoja aligeuka na kukimbia. Kisha mwengine, na mwengine. Hadi wote wakaenda zao.

Watu wa kijiji cha Balantu wakaokolewa.

Bibi akanyamaza. Wakati huu wote Sela alikuwa anashikilia shina la mbuyu.

"Kwa hivyo, ni mti huo uliowaokoa wanakijiji." Bibi akamaliza kuwahadithia.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Mti ulionusuru kijiji cha Balantu

Author - Karen von Wiese, Beryl Salt, Muhdni Grimwood and Barbara Meyerowitz
Translation - Mutugi Kamundi
Illustration - Julia te Water Naude
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© Karen Von Wiese, Beryl Salt, Mudhni Grimwood, Barbara Meyerowitz 1988
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org



Mwalimu Goso

Adapted from one of George W Bateman's Zanzibar Tales Versioned by Mitugi Kamundi
Jemma Kahn

Kiswahili



Hapo zamani kulikuwa na mwalimu aliyeitwa Goso.

Aliwafundishia wanafunzi chini ya mbuyu badala ya darasani.



Siku moja, paa alipanda juu ya mbuyu kuiba matunda.

Alitikisa tawi la mbuyu na tunda moja likamwangukia Mwalimu Goso.

Mwalimu Goso alifariki papo hapo.



Watoto walipofika chini ya mti walimpata mwalimu wao akiwa amekufa.

Walihuzunika sana wakataka kujua kilichomuua Mwalimu Goso.

Waliushika upepo wa kusini, "Ni wewe uliyeangusha tunda lililomgonga Mwalimu Goso. Hayo ni makosa makubwa."

Upepo wa kusini ulijibu, "Ningekuwa na nguvu kiasi hicho, ukuta wa matope ungewezaje kunikinga?"

Walikwenda kwenye ukuta wa matope, "Ni wewe uliyekinga upepo wa kusini ulioangusha tunda, lililomwangukia Mwalimu Goso. Hayo ni makosa makubwa."

Upepo wa kusini ulijibu, "Ningekuwa na nguvu kiasi hicho, panya angewezaje kutoboa shimo ubavuni mwangu?"

Walikwenda kwa panya, "Ni wewe uliyetoboa shimo kwenye ukuta wa matope, ambao ulikinga upepo wa kusini, ulioangusha tunda lililomwangukia Mwalimu Goso. Hayo ni makosa makubwa."

Lakini panya alijibu, "Ningekuwa na nguvu kiasi hicho, paka angewezaje kunila?"



Walimwambia paka, "Ni wewe humla panya, anayetoboa shimo kwenye ukuta wa matope, ambao ulikinga upepo wa kusini, ulioangusha tunda lililomwangukia Mwalimu Goso. Hayo ni makosa makubwa."

Lakini paka alijibu, "Ningekuwa na uwezo kiasi hicho, ningewezaje kufungwa kwa kamba?"

Waliiambia Kamba, "Ni wewe humfunga paka, ambaye hula panya anayetoboa shimo ubavuni mwa ukuta wa matope, uliokinga Upepo wa Kusini ambao uliangusha tunda lililomwangukia Mwalimu Goso. Hayo ni makosa makubwa."

Kamba ikasema, "Ningekuwa na uwezo kiasi hicho, ningewezaje kukatwa kwa kisu?"



Walikiambia kisu, "Ni wewe hukata Kamba, ambayo hufunga Paka, ambaye hula panya, ambaye hutoboa shimo ubavuni mwa ukuta wa matope, ambao ulikinga upepo wa kusini, ulioliangusha tunda, ambalo lilimwangukia Mwalimu Goso. Hayo ni makosa makubwa."

Kisu kilisema, "Ningekuwa na uwezo kiasi hicho, ningewezaje kuchomwa kwa moto?"

Basi wakaenda kwa moto, "Ni wewe huchoma Kisu, kinachokata kamba, ambayo hufunga paka, ambaye hula panya, ambaye hutoboa shimo kwenye ukuta wa matope, ambao ulikinga upepo wa kusini, ambao uliangusha tunda lililomwangukia Mwalimu Goso. Hayo ni makosa makubwa."

Moto ulisema, "Ningekuwa na uwezo kiasi hicho, ningewezaje kuzimwa na maji?"



Waliyaambia maji, "Ni wewe ambaye huzima moto, ambao huchoma kisu, ambacho hukata Kamba, ambayo hufunga paka, ambaye hula panya, ambaye hutoboa ukuta wa matope, ambao ulikinga upepo wa kusini ambao uliangusha tunda, ambalo lilimwangukia Mwalimu Goso. Hayo ni makosa makubwa."

Lakini maji yakasema, "Ningekuwa na uwezo kiasi hicho, ningewezaje kunywewa na ng'ombe?"



Walikwenda kwa ng'ombe, "Ni wewe ambaye hunywa maji, ambayo huzima moto, ambao huchoma kisu, ambacho hukata kamba, ambayo hufunga paka, ambaye hula panya, ambaye hutoboa ukuta wa matope, ambao ulikinga upepo wa kusini, ambao uliangusha tunda ambalo lilimwangukia Mwalimu Goso. Hayo ni makosa makubwa."

Lakini ng'ombe akasema, "Ningekuwa na uwezo kiasi hicho, ningewezaje kuumwa na mbung'o?"

Basi wakaenda kwa mbung'o, "Ni wewe ambaye humwuma ng'ombe, ambaye hunywa maji, ambayo huzima moto, ambao huchoma kisu, ambacho hukata Kamba, ambayo hufunga paka, ambaye hula panya, ambaye hutoboa ukuta wa matope, ambao ulikinga upepo wa kusini, ambao uliangusha tunda ambalo lilimwangukia Mwalimu Goso. Hayo ni makosa makubwa."

Mbung'o akasema, "Ningekuwa na uwezo kiasi hicho, ningewezaje kuliwa na paa?"

Basi wakampata paa, "Ni wewe ambaye hula mbung'o, ambaye humwuma ng'ombe, ambaye hunywa maji, ambayo huzima moto, ambao huchoma Kisu, ambacho hukata kamba, ambayo hufunga paka, ambaye hula panya, ambaye hutoboa ukuta wa matope, ambao ulikinga upepo wa kusini ambao uliangusha tunda, ambalo lilimwangukia Mwalimu Goso. Hayo ni makosa makubwa."



Paa alishtuka kwamba alikuwa ametambulika. Kwa hivyo, hakuwa na cha kusema.

Kisha watoto wakasema, "Ni wewe uliyeangusha tunda lililomgonga Mwalimu Goso. Ni wewe unayepaswa kuadhibiwa!"

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Mwalimu Goso

Author - Adapted from one of George W Bateman's Zanzibar Tales Versioned by Mitugi Kamundi
Illustration - Jemma Kahn
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© Adapted From One of George W Bateman'S Zanzibar Talestranslated By Mitugi Kamundi 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org

Ndalo na Pendo – Marafiki wakubwa

Ursula Nafula
Rob Owen

Kiswahili

African Storybook.org

Ndalo ana umri wa miaka 10. Yuko katika darasa la 5 katika shule iliyo pale kijijini. Ndalo huibuka wa kwanza darasani kwake. "Ni nini siri yake?" Wenzake wanajiuliza.

Ndalo anasoma na kuandika vizuri. "Je, anawezaje kufanya hivi?" Wanashangaa. Ndalo anawaeleza kwamba ni kwa sababu ana vitabu vingi. Wao wanapopoteza muda wao wakikaa bila kazi, yeye huutumia muda wake kusoma.

Wakati mwingine Ndalo hupata Shilingi 80 kama pesa za matumizi. Yeye huzitumia pesa zake nyingi kununua vitabu kutoka duka la vitabu vikuukuu lilioko pale kijijini.

Je, Ndalo hupataje pesa za matumizi anazotumia kununua vitabu? Fungua ukurasa ufuatao upate kujua.



Huyu ni Pendo, ng'ombe wa maziwa. Yeye hutoa maziwa lita 20 kwa siku. Babake Ndalo huuza maziwa hayo.

Ng'ombe huhitaji chakula na maji. Vilevile, huhitaji kutembea uwanjani. Kwa hivyo, kila siku baada ya kutoka shuleni, Ndalo hufanya kazi hiyo. Babake humpatia pesa za matumizi kwa kazi hiyo. Ni pesa hizo ambazo Ndalo huweka kwa ununuzi wa vitabu kila juma.

Kwanza, Ndalo humpa Pendo karoti 8 kila siku. Kila siku yeye huzichuma karoti kutoka kwenye bustani ya babake.

Ukifanya hesabu, utapata kwamba Pendo hula takriban karoti 60 kwa juma. Je, unaweza kupata hasebu kamili?



Baada ya hiyo, Ndalo humpeleka Pendo malishoni. Babake alimwonya achunge ili Pendo asile nyasi kwa zaidi ya robo tatu ya saa.

Kawaida, Pendo huanza kula nyasi saa nane na dakika kumi na tano ili Ndalo aweze kumrudisha saa tisa kwenye kibanda cha kukamulia. Wakati wa majira ya baridi, ambapo giza huingia mapema, Ndalo huweza kuanza kula saa saba na nusu.

Baada ya hilo, Ndalo humpa Pendo maji. Bila maji Pendo hawezi kutoa maziwa hata Ndalo akimlisha
namna gani. Ndalo husomba maji kwa ndoo kutoka mfereji ulio pale kijijini kwa sababu hakuna mwingine ulio karibu.

Hori la Pendo huweza kubeba maji lita 30. Ndoo ya Ndalo hubeba tu lita 5 peke yake. Kwa hivyo ili ajaze hori, Ndalo huenda mara chache. Je, unaweza kufanya hesabu ya jumla ya safari zote?

Halafu, Ndalo humpeleka Pendo ili apate nafaka yake ya kila siku ya kilo 12. Ndalo akihesabu, anapata jumla ya kilo 90 kwa juma.

Kila gunia linagharimu Shilingi 39. Ndalo anafanya hesabu ya nafaka ya kila juma. Kwanza anafanya hesabu ya magunia 7 kwa Shilingi 40 kila gunia. Anapata jumla ya Shilingi 280. Kisha anaondoa Shilingi 7 na kubaki na salio la Shilingi 273. "Hiyo ni kama Shilingi 10 000 kwa mwaka!" Ndalo anakadiria. Je, hiyo ni sawa?

Babake Ndalo anamkama Pendo mara mbili kwa siku. Pendo hutoa maziwa lita 24 kwa siku, kwa hivyo hutoa karibu lita 12 kila anapokamuliwa.

Wakati mwingine Ndalo husaidia kukamua lakini, si kazi rahisi kama inavyoonekana. "Siku moja, nitakuwa na ng'ombe wangu mwenyewe ambao nitalazimika kukamua mwenyewe," Ndalo anawaza.

Babake anayamwaga maziwa kwenye ndoo ndogo ya lita 2. Vilevile, anayamwaga kwenye chupa za lita 1. Halafu anayauza maziwa hayo kwa Shilingi 8 kwa kila lita.

Mara moja kwa juma, babake Ndalo huchanga lita 25 za maziwa kusaidia mpango wa chakula shuleni. Hii ina maana kuwa watoto 100 hupata maziwa siku hiyo.

Kwa kila lita inayouzwa, babake anampa Ndalo senti 50. Hiyo haionekani kuwa nyingi, lakini ikiwa babake anauza lita 24 kwa siku, hizo senti huongezeka na kuwa pesa nyingi. Je, unaweza kufanya hesabu na kujua kiasi kamili?

Ndalo anaziweka hela zake hadi Jumamosi wakati anapolitembelea duka la vitabu. Kila kitabu kinagharimu chini ya shilingi 10. Kwa hivyo, anaweza kununua vitabu vingi katika juma moja.

Ndalo pia hupenda kuyanywa maziwa anayotoa Pendo. Babake husema kwamba maziwa husaidia kujenga mifupa na meno na kuipa nguvu. Pia humpa mtu afya nzuri.

Kwa kuwa anayanywa maziwa na kuzila mboga nyingi kutoka bustani ya babake, Ndalo ana nguvu na mwenye afya nzuri. Ni nadra yeye augue au ahisi njaa.

Ndalo hasahau kumshukuru Pendo mwishoni mwa siku. Humzawadi kwa kumpatia karoti zaidi au matawi ya mchicha yapatikanayo kwenye bustani.

"Asante Pendo, wewe ni rafiki yangu mkubwa! Mimi ni mwenye nguvu, mwenye afya na mwerevu kwa ajili yako. Usingekuwa wewe, nisingeweza kuvinunua vitabu vinavyonisaidia kuibuka wa kwanza darasani."

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Ndalo na Pendo – Marafiki wakubwa

Author - Ruth Odondi
Translation - Ursula Nafula
Illustration - Rob Owen
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative and Molteno Institute, 2017
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org

Ndege-Asali alipiza kisasi

Brigid Simiyu
Wiehan de Jager

Kiswahili

African Storybook.org

Hii ni hadithi ya Ndege-Asali na mvulana mmoja mlafi aliyeitwa Jeuri. Siku moja Jeuri alipokuwa akiwinda, alisikia mwito wa Ndege-Asali amabye huwaongoza watu palipo na asali.

Jeuri alianza kudondokwa na mate alipofikiria juu ya asali. Alisikiliza na kutazama vizuri hadi akamwona Ndege-Asali aliyekuwa ametua kwenye matawi.

"Chitik-chitik-chitik," Ndege-Asali aliruka na kutua kwenye mti uliokuwa karibu. "Chitik-chitik-chitik," aliita, huku akinyamaza na kuhakikisha kwamba Jeuri alikuwa amemfuata.

Baada ya nusu saa, waliufikia mti wa mtini.

Ndege-Asali aliruka kama mwenda wazimu kutoka tawi moja hadi nyingine.

Jeuri alisimama akamtazama kwa muda mrefu.

Baadaye, Ndege-Asali alitulia kwenye tawi moja, akageuza kichwa chake na kumwangalia Jeuri.

Jeuri aliamini kuwa Ndege-Asali alikuwa akisema, "Asali iko hapa! Njoo sasa!"

Jeuri hakuweza kuwaona nyuki wowote kutoka chini ya mti kwa vile alimwamini Ndege-Asali.

Jeuri aliuweka mkuki wake chini ya mti. Akakusanya vijiti vilivyokauka kisha akakoka moto mdogo.

Moto ulipowaka vizuri, Jeuri alikitia kijiti kirefu kilichoaminika kutoa moshi mwingi.

Alianza kukwea mti akiwa amekishika kwa meno.

Baadaye, Jeuri alisikia sauti ya nyuki. Walikuwa wakiingia na kutoka mzingani. Alipoufikia mzinga, alikisukuma ndani kile kijiti kilichokuwa na moto.

Nyuki walitoka ndani kwa hasira wakihisi uchungu. Waliruka na kwenda kwa sababu hawakupenda moshi.

Hata hivyo, walifanya hivyo tu baada ya kumuuma Jeuri!

Nyuki walipokuwa nje, Jeuri aliingiza mkono wake ndani ya mzinga.

Alitoa kipande kikubwa cha asali iliyokuwa ikidondoka. Aliiweka kwa utaratibu ndani ya mkoba aliokuwa nao na kuanza kushuka.

Ndege-Asali alishuhudia kila kitendo alichofanya Jeuri. Alikuwa akisubiri kubakishiwa kiasi kidogo cha asali kama shukurani kwa kumwongoza Jeuri kwenye asali.

Aliruka kutoka tawi hadi tawi huku akikaribia chini.

Mwishowe Jeuri alifika chini. Ndege-Asali alitua kwenye jiwe karibu na Jeuri akisubiri zawadi yake.

Lakini Jeuri aliuzima moto, akachukua mkuki wake na kuanza safari bila kumjali Ndege-Asali.

Ndege-Asali aliita kwa hasira, "USH-ndi! USH-ndi!" Jeuri alisimama, akamkodolea macho kisha akacheka kwa sauti. "Rafiki yangu, unataka asali kidogo? Ha! Mimi ndiye nilifanya kazi yote pamoja na kuumwa na nyuki. Kwa nini nikugawie asali hii tamu?"

Jeuri aliondoka na kwenda zake.

Ndege-Asali alikasirika sana! Hivi sivyo ndivyo alistahili kutendewa!

Lakini, atalipiza kisasi.

Siku chache baadaye, Jeuri alisikia tena mwito wa Ndege-Asali uliohusu asali. Aliikumbuka asali tamu, na kwa mara nyingine, alimfuata kwa hamu.

Baada ya kumwongoza Jeuri kwenye msitu, Ndege-Asali alipumzika chini ya mti wa mwavuli. "Aa, bila shaka mzinga umo ndani ya mti huu," Jeuri aliwaza.

Kwa haraka, aliwasha moto wake na kuanza kukwea mti akiwa amebeba kuni iliyotoa moshi.

Ndege-Asali alimtazama tu.



Jeuri alipopanda, alishangaa kwa nini hakusikia sauti ya nyuki. "Pengine mzinga umefichika ndani ya mti zaidi," alifikiria.

Alipanda tena juu ya tawi jingine. Lakini badala ya mzinga, alijikuta akiwa ana kwa ana na Chui!



Chui alikuwa na hasira sana kwa sababu usingizi wake ulikuwa umekatizwa.

Aliiyafanya macho yake yakawa madogo, akaufungua mdomo wake na kuyaonyesha meno yake makubwa makali.

Kabla ya Chui kumvamia, Jeuri alishuka haraka chini. Katika haraka hiyo, aliteleza na kuanguka kwa kishindo akaumia mguu wake.

Alirukaruka akienda kwa haraka alivyoweza. Kwa bahati nzuri, Chui alikuwa bado akihisi usingizi, kwa hivyo hakumfukuza.

Ndege-Asali alikuwa amelipiza kisasi na Jeuri alikuwa amejifunza funzo lake.

Kwa hivyo, watoto wa Jeuri na watoto wa watoto wao wanamheshimu sana Ndege-Asali wanapoisikia hadithi yake ya kuwaongoza watu kwenye asali.

Kila wanapotoa asali, wao huhakikisha kwamba wanamzawadi kwa kiasi kikubwa cha asali!

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Ndege-Asali alipiza kisasi

Author - Zulu folktale
Translation - Brigid Simiyu
Illustration - Wiehan de Jager
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org

Ndizi za Bibi

Peter Chege
Catherine Groenewald

Kiswahili

African Storybook.org

Bibi alikuwa na shamba lenye rutuba lililojaa mtama, mawele, mihogo, na zaidi ya yote, ndizi.

Ingawa Bibi alikuwa na wajukuu wengi, nilijua alinipenda zaidi. Alinikaribisha nyumbani kwake mara kwa mara na kunifichulia siri zake.

Lakini, kulikuwa na siri moja aliyokataa kunifichulia. Hakunifichuliwa alivyoziivisha ndizi zake.

Siku moja, niliona kapu kubwa limeanikwa nje ya nyumba ya Bibi. Nilipomwuliza kapu lilikuwa la nini, alinijibu, "Hili ni kapu langu la ajabu."

Kando ya kapu lile, paliwekwa majani ya mgomba. Bibi alikuwa akiyageuzageuza. Nilijawa na shauku nikauliza, "Bibi, majani haya ni ya nini?"

Bibi alinjibu, "Ni majani yangu ya ajabu."

Nilifurahia kumtazama bibi, zile ndizi, yale majani ya mgomba na lile kapu kubwa.

Bibi alinituma kwa mamangu. "Bibi, tafadhali niruhusu nione unavyotayarisha."

"Mwana wee, usiwe mtundu, fanya ninavyokwambia,"Bibi alinifokea.

Niliondoka mbio.

Niliporudi, nilimpata bibi amekaa nje. Hapakuwa na kapu wala zile ndizi.

"Bibi, li wapi kapu, zi wapi ndizi, na ya wapi..?"

"Zipo mahali pangu pa ajabu," Bibi alijibu.

Jibu lake lilinivunja moyo.

Siku mbili baadaye, Bibi alinituma nimchukulie mkongojo wake kutoka chumbani. Mara tu nilipoufungua mlango, nilikaribishwa na harufu tamu ya ndizi mbivu.

Kapu kubwa la ajabu la Bibi lilikuwa kwenye chumba cha ndani. Lilifunikwa kwa blanketi kuukuu.

Nililifunua blanketi na kunukia harufu tamu.

Nilibumburushwa na sauti ya Bibi akiita, "Wafanyaje wewe? Niletee mkongojo haraka."

Nilitoka haraka kumpelekea mkongojo. "Tabasamu ni la nini?" Aliniuliza Bibi.

Swali lake lilinikumbusha kuwa nilikuwa bado ninatabasamu kwa kupavumbua mahali pake pa ajabu.

Keshoye, Bibi alipokuja kumuamkua mama, nilichapuka na kwenda nyumbani kwake kuziangalia zile ndizi tena.

Palikuwa na kichala kimoja cha ndizi zilizoiva. Nilichuna moja na kuificha rindani mwangu. Nililifunika kapu, nikaenda nyuma ya nyumba, nikaila ndizi kwa haraka.

Ilikuwa tamu ajabu.

Siku iliyofuata, Bibi alipokuwa kitaluni akichuma mboga, nilipenya haraka nikazichungulia ndizi. Karibu ndizi zote zilikuwa zimeiva.

Nikakichukuwa kichala cha ndizi nne. Nilipokuwa nikinyemelea kuelekea mlangoni, nilimsikia Bibi akikohoa.

Niliwahi kuzificha rindani na nikampita nikelekea nje.

Siku iliyofuata, ilikuwa siku ya soko. Bibi aliamka alfajiri mapema. Kila mara aliziuza ndizi na mihogo sokoni.

Siku hiyo, sikuharakisha kumtembelea. Ingawa hivyo, singeweza kumuepuka kwa muda mrefu.

Siku hiyo jioni, Baba, Mama na Bibi waliinita. Nilijua sababu.

Usiku ule nilipokuwa nimelala, nilijua singewahi kuiba tena, si kutoka kwa Bibi, si kutoka kwa wazazi wangu, wala kutoka kwa mtu yeyote.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Ndizi za Bibi

Author - Ursula Nafula
Translation - Peter Chege, Alice Karichi, Michael Muriuki and Ursula Nafula
Illustration - Catherine Groenewald
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org

Refi awaosha kuku wake

Brigid Simiyu
Wiehan de Jager

Kiswahili

African Storybook.org

Ilikuwa harusi ya kwanza katika familia ya Tenana. Refi alikuwa amechangamka sana.

"Nitakuwa msaidizi wa Elsa nikiwa nimevaa nguo na viatu vipya!" Refi aliwaelezea kuku wake. Aliwaelezea kuku wake kila kitu.

Babake alikuwa amempa kuku kama zawadi alipokuwa akiadhimisha siku ya kuzaliwa kwake. Refi aliwapenda sana.

"Refi, waondoshe hapo hao kuku wachafu!" Mamake alipiga kelele, "Siwataki popote karibu na hema la harusi."

Refi aliwafukuza kuku kutoka kwenye hema. "Tokeni enyi viumbe washienzi," alisema. "Singependa mliwe wakati wa harusi ya Elsa."

"Mama asema kwamba hii itakuwa harusi ya kufana zaidi katika kijiji cha Mailisaba," Refi aliwaambia kuku wake. "Pia anasema kwamba ninaweza kuwasaidia wasichana wale wakubwa kupika." Kuku hawakumsikiliza hata kidogo.

"Refi!" Mamake alimwita kutoka ndani, "Tafadhali acha hao kuku. Njoo unichungie chungu!"

Mamake Refi alijivunia nyumba yake na alitaka iwe safi siku ya harusi. Alisafisha, akaosha na kusugua kila kilochokuwamo. Alipomaliza, hapakuwa na chembe cha vumbi popote.

Kuku walipochokoa vichwa mlangoni, Mamake Refi alipiga mayowe, "Tokeni nje ninyi viumbe vyenye miguu na midomo michafu!"

Refi aliwafuata kuku wake hadi kwenye jua. "Mama anasema ukweli, mnaaibisha," aliwakemea.

Refi alitabasamu kisha akaenda kujaza ndoo maji. Alikuwa na wakati mgumu kuwashika kuku wake. Hawakudhani kwamba ilikuwa jambo zuri wao kuoga.



Refi alimweka kuku wa kwanza ndani ya ndoo ya maji. "Kaa wima, ewe kiumbe shenzi," alipiga kelele. "Haitachukua muda mrefu kukuosha!"



Refi alipopangusa pua na macho ya kuku, ghafla kuku alikuwa dhaifu akaanguka kando ya ndoo. "Huu sio wakati wa kulala," Refi alisema.

Alimtikisa kuku kwa nguvu ili maji yote yadondoke. Kisha akamlaza juu ya nyasi ili akauke. Kuku alitulia pale akiwa amelala.



Aliwaosha kuku wote wanane na kuwaweka mstari mmoja juu ya nyasi ili wakauke. Hakuna yeyote aliyepapatua hata unyoya mmoja.

"Nitawaacha mlale kwa muda mfupi," Refi aliwaza. Alienda kukitazama chungu kilichokuwa mekoni.

Shangazi zake Refi, yaani Mama Netty na Mama Teddy, walikuwa wakitayarisha harusi ya Elsa.

Walitakiwa kufanya matayarisho hayo kwa pamoja lakini hawakupendana hata kidogo.

Mama Netty aliwaona kuku wa Refi wakiwa wanakauka. "Hiki ni chakula kizuri kwangu. Nitawapeleka nyumbani!" Alijiambia.

Alilichukua kanga lake na kuwafungia kuku wote mle ndani. Hakuna kuku hata mmoja aliyesonga. "Sawa kabisa!" Alitabasamu. "Sasa nitawaweka mahali ambapo Mamake Teddy hatawahi kuwapata."

Alikiweka kifurushi hicho pembeni kati ya maboga."

Mama Teddy aliamua kutayarisha kitoweo alichokipenda. Alikwenda katika bustani ya maboga. Alikiona kifurushi cha Mama Netty chini ya mboga.

Alipokifungua, kuku wote wanane walianguka nje. "Esh!" Alipiga kelele huku akiruka nyuma kwa mshangao. "Ah, ninyi ndio kuku wasafi kuliko wote! Mko tayari kwa chungu changu," aliwabembeleza. "Sasa nitawaficha wapi wapenzi wangu?" Mama Teddy alicheka. "Lazima nipate mahali pazuri kabisa," alisema huku akitembea nyumbani.



"Ninajua," alisema hatimaye, "Nitawaweka paani!" Mama Teddy alipanda juu akawaweka kuku katika mstari kwenye paa la nyumba ya nyasi.

Siku iliyofuata, jua lilichomoza kwa wakati mzuri kwa harusi. Refi alikuwa wa kwanza kuamka na kwenda kuwatazama kuku wake.

Hakuwapata mahali alikuwa amewaweka. "Lazima wawe wamekauka vizuri kwa sasa. Nina hakika wameenda kutafuta kifungua kinywa chao," alisema.

Harusi ya Elsa ilikuwa ya kufana. Wale kuku hawakuamka kutoka paani. Kwa hivyo, hawakujiunga na wasichana wasaidizi wa bi-harusi walipoingia wakicheza.

Hakuna kuku yeyote aliyetikisika wakati kwaya ya kanisa iliimba kwa sauti ya juu nyimbo nzuri za kuvutia. Walikuwa bado wanalala juu ya paa wakati Padre alihubiri.

Hawakutikisa hata unyoya wakati nguruwe na babu yake Refi walipokoroma mahubiri yalipoendelea.

Hakuna hata mguu mmoja wa kuku uliotetemeka wakati kondoo waliranda na kuingia ndani ya hema wakiwa karibu kuangusha keki ya harusi.

Wakati babake bwana harusi alipokuwa katikati ya hotuba yake ndipo mambo yalianza kubadilika paani.

Kuku wa kwanza aliyanyoosha mabawa yake na kuruka kwenye kifua cha Mamake Molly.

Mama Teddy aliyekuwa amekaa karibu naye alianza kucheka. Kuku mwingine alirukia kitambaa kipya cha Mama Netty. Watu waliokuwa kwenye meza nyingine walizuia kicheko.

Mwanamke aliyekaa karibu na Mama Netty aliweka kichwa chake chini ya meza, "Ai, aai, aaaaii, he, he, heeeeeeee!" Alicheka.

Wale kuku wote waliamua kujiunga na wale wawili wa kwanza.

Hungeweza kumwona Mama Netty kwa sababu alikuwa amefunikwa na kuku hao wote!

Wageni walicheka kwa mayowe. Wanaume walilazimika kuzishika tumbo zao. Wanawake waliviringika katika viti vyao.

Vijana walijishikilia kwa wenzao. Akina nyanya hawangeweza kupumua kwa ajili ya kucheka. Akina babu walitikisa fimbo zao.

Halafu, shangazi hao wawili walitazamana wakaanza kucheka pia.

Mama Teddy aliufungua mdomo wake wazi kwa kicheko.

Mama Netty alikirusha kichwa chake nyuma na kucheka hadi mashavu yakatikisika.

Refi hakuamini!

Wageni wote walikubaliana kwamba hiyo ilikuwa harusi nzuri zaidi iliyowahi kufanyika kijijini Mailisaba.

"Aa, mna bahati sana! Refi aliwaambia kuku wake alipokuwa anawaweka kwenye chumba chao usiku ule.

"Mama anasema kuwa hatawahi kuwaweka kwenye chungu chake."

"Lakini, tazama jinsi mlivyo wachafu tena," aliwaambia.

"Nadhani nitalazimika kuwaosha tena kesho!"

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Refi awaosha kuku wake

Author - Marion Drew
Translation - Brigid Simiyu
Illustration - Wiehan de Jager
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org

Samaki Mkarimu

Brigid Simiyu
Jemma Kahn

Kiswahili

African Storybook.org



Hapo zamani za kale, Mpunzi na mkewe waliishi na mtoto wao mmoja wa kike aliyeitwa Nosisa.

Mpunzi alitaka mtoto mvulana, lakini yeye na mkewe hawangeweza kupata watoto wengine.

Mpunzi alimlaumu mkewe kwa kutompa mtoto wa kiume.

Siku moja, Mpunzi alimchapa mkewe akatoroka na kwenda nyumbani kwao. Alihuzunika kwani Mpunzi hakumruhusu aende na Nosisa.

Mpunzi alimdhulumu bintiye namna alivyomfanyia mkewe. Nosisa aliishi maisha ya huzuni sana.

Mpunzi alioa mke mwingine. Alitumaini kwamba mke huyo mpya angemzalia mtoto mvulana.

Maisha ya Nosisa sasa yalikuwa magumu zaidi. Mpunzi alimtetesha na kumlazimisha kumtumikia mke wake mpya.

Nosisa alifanya kazi kama mtumwa.

Mpunzi aliona fahari sana kutokana na mifugo wake. Alizoea kutazama mifugo wake wakila nyasi uwanjani. Alihisi kuwa alikuwa ametosheka sana na mali yake.

Wengi wa wafanyakazi wa Mpunzi walisafisha makao yake na kuwachunga mifugo wake. Walikama maziwa ambayo Mpunzi aliwauzia wanakijiji.

Mpunzi alimpenda sana mke wake mpya. Alimchukulia kama malkia. Alikaa chumbani wakati wote huku akiwaamrisha Nosisa na wafanyakazi.

Nosisa alirauka mapema kila siku kumtayarishia chai mamake wa kambo. Alimfagilia chumba chake na kumpikia.

Lakini mamake wa kambo alinung'unika kuwa chakula chake kilikuwa baridi, kuwa chai yake ilikuwa hafifu, na kwamba chumba chake kilikuwa kichafu.

Siku moja Mpunzi alikasirika akamkaripia na kumgonga Nosisa kwa kijiti. Nosisa alitoroka akaenda mtoni alikokaa na kulia alasiri nzima.

Ghafla, alisikia sauti kutoka majini. Alimwona Samaki aliyekuwa akitoa ile sauti. Nosisa alishtuka lakini Samaki alimtuliza, "Tafadhali, binti yangu, usitoroke, mimi ni mamako. Nimebadilika kuwa samaki ili babako asinitambue."



"Una shida gani?" Samaki aliuliza. Nosisa alimweleza kuhusu maisha yake ya huzuni. "Usiwe na wasiwasi mwanangu. Nitakuletea chakula kila siku," Samaki alisema.

Alimpa Nosisa mboga wakasherehekea halafu akatokomea. Nosisa alienda nyumbani akiwa anatabasamu. Alijua hatalala tena njaa kama ilivyokuwa desturi.

Kila asubuhi Nosisa aliamka na kufanya kazi zote za nyumbani kama ilivyokuwa kawaida. Adhuhuri, alienda mtoni.

Aliita kila wakati, naye Samaki alitokea akiwa amebeba chakula kitamu. Nosisa alifurahi na kumwelezea chochote. Alianza kuwa na afya nzuri.



Nosisa alimtembelea Samaki kila siku hadi mamake wa kambo akaanza kumshuku. "Kuna jambo linaendelea kule mtoni, na ni lazima nitaligundua," aliwaza.

Alasiri moja alimfuata Nosisa hadi mtoni. Alimwona Nosisa akimzungumzia Samaki na kupokea chakula kitamu. Siri ya Nosisa sasa ilikuwa imetambulika!

"Lazima nifanye jambo kumhusu huyu samaki," alisema mama wa kambo.



Mpunzi aliporejea jioni, alimpata mkewe mpya akiwa chumbani kwake akilia. "Unasumbuliwa na nini mke wangu mrembo?" Mpunzi aliuliza.

"Mganga aliniambia kwamba njia pekee ya kukuzalia mtoto mvulana ni kumla samaki mkubwa aishiye kwenye mto ulio karibu hapa," alisema. "Je, utaniletea samaki huyo usiku wa leo?" mwanamke akamsihi.

"Nitakufanyia lolote," Mpunzi akasema.

Mpunzi alianza safari ya kwenda mtoni kabla giza kuingia. Aliwachukua wafanyakazi wake ili wamsaidie. Mpunzi alimpata samaki mkubwa zaidi.

Alipofika nyumbani, moto mkubwa wa kumpika yule samaki ulikuwa tayari. "Nitatayarisha kitoweo kizuri," mwanamke akamwelezea Mpunzi aliyekuwa amefurahi sana.



Usiku ule Mpunzi na mkewe walienda kulala baada ya chakula kitamu. Waliacha mifupa mezani ili Nosisa asafishe asubuhi yake.

Nosisa alipowaletea kahawa chumbani, walikuwa bado wanalala. "Hili ni jambo geni," Nosisa alifikiria. "Babangu huamka mapema mno kwenda kazini. Kwa nini leo bado analala?"



"Heri nikimbie mtoni nipate kiamsha kinywa kizuri," alifikiria. Nosisa alikimbia kwenda mtoni. Alipofika kule, alimwita Samaki mara nyingi lakini Samaki hakuja.

Nosisa alianza kulia. Hakujua kilichotokea. Alipokuwa akilia, ndege mmoja alimwambia kilichotendeka. Alilia kwa nguvu akidhani kwamba mamake alikuwa ameangamizwa.



Ndege alimwambia aiokote mifupa kutoka mezani kisha airushe mtoni. Angefanya hivyo, Samaki angefufuka.

Alimwambia pia awaache babake na mamake wa kambo walale hadi adhuhuri.

Nosisa alifanya alivyoambiwa. Aliichukuwa mifupa, akaiweka mfukoni kisha akairusha mtoni.

Nosisa alikimbia kurudi nyumbani na kabla adhuhuri kufika, aliwaamsha baba na mamake wa kambo.

Hakuwatambua! Walikuwa wamezeeka na kudhoofika. Hawangemkaripia wala kumpiga tena. Walichoka wasiweze kuuchunga mji wao.

Nosisa aliichukua mali ya babake. Akawaita wafanyakazi wote na kuwaambia kilichotokea. Wakasherehekea na kuishi kwa amani.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Samaki Mkarimu

Author - Kholeka Mabeta
Translation - Brigid Simiyu
Illustration - Jemma Kahn and Wiehan de Jager
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org

Tembo Mdogo

Ben Terarc
Ben Terarc

Kiswahili

African Storybook.org



Tembo Mdogo alikuwa akitembea porini na mamake na dadake mkubwa. Walikuwa wakiimba kwa sauti na kurusha vumbi.

Kwa bahati mbaya, Tembo Mdogo akajikwaa kwenye jiwe na hakuweza kutembea tena. Alibaki nyuma.

Mama na dada waliendelea bila kujua kama Tembo Mdogo alikuwa amebaki nyuma.

Tembo Mdogo hakujua pa kuenda. Alianza kulia kwa uoga.

Kwa bahati nzuri Panda alikuwa ndani ya majani karibu na mahali ambako Tembo Mdogo alikuwa ameketi chini.

Panda alimsongea akamwambia, "Nifuate. Mahali hapa kuna wanyama wengine ambao wanaweza kukuumiza."

Tembo Mdogo hakusita kukubali kwa sababu hakuwa na mahali pengine pa kuenda. Vilevile kijiji chake kilikuwa mbali.

Walipofika katika kijiji cha Panda, kila mnyama alionyesha uso tofauti. Baadhi ya wanyama walimpenda Tembo Mdogo. Wengine walikasirika na wengine wakaogopa. Hawakujua jinsi mfalme wao Simba angeamua.

Kwa kweli Simba hakukubali Tembo Mdogo abaki katika Kijiji kile. Alisema, "Atakayepinga uamuzi wangu, atafukuzwa pomoja na Tembo Mdogo. Ufalme wangu si wa watu wa nje ila ni wa vizazi vya hapa.

Simba alimwambia Tembo Mdogo, "Nenda mbali au niivunje mifupa yako mara mia."

Tembo Mdogo alishtuka akakosa la kusema. Akaamua kuenda. Lakini, rafiki yake Panda akaona hawezi kumuacha aende peke yake.

Kwa ajili ya upendo aliokuwa nao kwa Tembo Mdogo, Panda aliacha kila kitu na kumrudisha nyumbani.

Tembo Mdogo alifurahi sana hata akambeba mgongoni.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Tembo Mdogo

Author - Ben Terarc
Illustration - Ben Terarc
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2018
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org

Theuri amwokoa Kobani!

Ursula Nafula
Catherine Groenewald

Kiswahili

African Storybook.org

Kobani alikuwa mwanamume mrefu sana. Wanakijiji walimwita Kobani, Muungwana, kwa sababu alikuwa mpole na rafiki wa watu. Hakuwa kama watu wengine wakubwa tunaosoma juu yao katika hadithi za kutisha.

Wakati wa mchana, Kobani alifanya kazi yake shambani. Mpini wa jembe lake ulikuwa mfupi mno kwa hivyo alilazimika kuinama hadi chini kuifanya kazi yake. Bila shaka, mgongo wake ulikuwa na maumivu mengi kutokana na kuinama kwingi.

Theuri aliishi karibu na Kobani. Alihuzunika sana alipomwona Kobani akipambana na jembe lake lenye mpini mfupi au alipoinama chini ili apite mlangoni kwake.

Theuri aliamua kumsaidia Kobani. Alizungumza na wazee wa kijiji na kuwauliza usaidizi. Lakini, kabla wao kufanya hivyo, walitaka kujua urefu kamili wa Kobani.



Theuri alimwuliza Kobani, "Wewe ni mrefu kiasi gani?" Kobani alikisia akasema, "Nadhani urefu wangu ni mita 2.5." Kobani alilala kitandani halafu akamweleza, "Ninajua godoro langu ni refu mita 1.5. Unaona hata miguu yangu inaning'inia mwisho karibu mita nyingine. Hiyo ina maana kuwa mimi ni mrefu mita 2.5."

Sasa Theuri angeweza kuwaeleza wazee kwamba Kobani ni mrefu mita 2.5. Alikuwa mrefu kweli!

Theuri angeweza kuanza kutekeleza mpango wake wa siri.

Theuri, Kobani na Choke, kipenzi chake, waliondoka kwenda sokoni. Waliitumia baiskeli ya Kobani iliyokuwa ndogo. Kobani alilazimika kuunyoosha mguu wake ili aweze kuiendesha ile baiskeli. Theuri aliketi kikapuni akiogopa kutazama barabara namna baiskeli ilivyoyumbayumba kila upande.



Waliposhuka sokoni, umati wa wanakijiji ulimzunguka Kobani. Chifu wa kijiji alimkaribisha. "Hujambo Bwana Muungwana. Theuri alitueleza kuwa unakumbwa na matatizo maishani mwako kutokana na urefu wako," Chifu alisema.

Aliendelea kumwambia, "Tunataka kukusaidia. Tutahakikisha kuwa kila kitu unachohitaji kinakufaa. Hivi karibuni, matatizo yako yatazikwa katika kaburi la sahau. Subiri tu ujionee."

Wanakijiji walifanya kazi mfululizo kuhakikisha kuwa chochote Kobani alihitaji kilikuwa kimetengenezwa kwa kimo kilichomfaa.

Litazame jembe hili. Ulinganishe mpini wa jembe jipya na ule mzee. Mpini mpya unaonekana kuwa mrefu mara mbili. Unadhani hilo jembe jipya ni refu kiasi gani? Zaidi ya mita moja? Chini ya mita mbili?

Baadaye, wanakijiji walimsaidia Kobani kutengeneza fremu refu na mlango mpya uliokuwa mrefu. Fremu ilikuwa ndefu kumliko Kobani ili asiiname sana atakapokuwa akiingia nyumbani. Ilikuwa ya kumfaa hasa!

Hebu ichunguze ile picha kwa makini. Urefu wa Kobani ni takriban mita 2.5. Je, unadhani fremu ya mlango wake mpya ni refu kiasi gani?



Halafu walitengeneza kitanda kipya na godoro lililokuwa refu zaidi. Vilevile walinunua shuka na blanketi ya kuufunika mwili wa Kobani kutoka kichwani hadi miguuni.

Sasa, Kobani angetazamia kulala usingizi kwa amani. Miguu yake haitaning'inia kando ya godoro tena. Tazama jinsi mwili wake ulivyofunikwa kabisa. Hata kuna nafasi iliyobaki upande mmoja wa kitanda.

Chifu alimwuliza mmoja wa wahunzi wa mle kijijini
kumtengenezea Kobani baiskeli kubwa. Baiskeli hiyo ilikuwa na kikapu kikubwa ambamo Theuri na Choke wangeketi.

Kila sehemu ya baiskeli hiyo ilikuwa kimo cha kumfaa Kobani. Kobani hakuhitajika tena kuikokota miguu yake barabarani wala kuining'iniza kando ya baiskeli.



Maseremala walimtengenezea Kobani meza mpya iliyokuwa na miguu mirefu ya mita 1.5. Sasa anapoketi kula, miguu yake inagusa chini.

Theuri huketi kwenye kigoda kirefu karibu naye. Yeye huhitaji ngazi ili afike juu. Hesabu vidato ambavyo Theuri anastihili kupanda ili amfikie Kobani. Je, unadhani ngazi hiyo ni refu kiasi gani?

Jembe jipya la Kobani humwezesha kupanda mimea na kuvuna kwa urahisi. Bustani yake ilibadilika na kuwa msitu! Kobani huwaachia wanakijiji vikapu vya matunda mbele ya mlango wa nyumba yake kuonyesha shukuruni zake kwa msaada wao.

Na hili lilianza na ndoto aliyokuwa nayo Theuri ya kutaka kumrahisishia maisha rafiki yake, Kobani Muungwana.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Theuri amwokoa Kobani!

Author - Cornelius Gulere
Translation - Ursula Nafula
Illustration - Catherine Groenewald
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative, 2017
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org
Original source www.ugcla.org



Uamsho wa furaha

Brigid Simiyu
Catherine Groenewald

Kiswahili

African Storybook.org

Kwa muda mrefu Mlima Olokwango ulisimama akitabasamu katikati ya sehemu Tambarare ya Kwere.

Kutoka kwa vibonyeo viwili vilivyokuwa pembeni mwake, kulitoka vijito vilivyokaribiana na kuunda mto.

Mambo yalikuwa swari hadi Matata alipokuwa mkuu wa mahali hapo.

Alilazimisha njia itengenezwe kutoka juu ya mlima hadi chini yake ili aweze kupanda kwa urahisi na kujifiringisha hadi chini.

Mlima Olokwango ulikasirika na uharibifu uliofanywa lakini ulivumilia.



Kila wikendi, watoto wa Matata na marafiki zao wangepanda mlimani kucheza.

Wangekimbia kila mahali huku wakivunja vijiti na matawi, wakiwasha mioto kwa michezo yao ambao baadaye, waliiacha ikiwaka.



Mlima Olokwango ulipoteza uvumilivu wake. Tabasamu yake nzuri ilififia. Vibonyeo viliendelea kuwa vidogo jinsi uso wake ulivyokuwa na mikunjo.

Mwishowe, vijito havikuwa tena. Kingo za Mto Temu zilihuzunika. Paa walihama kwani hapakuwa tena na zile nyasi ndefu za kijani walizochezea ndani wala kulala juu yake.

Mifugo, walikonda na kukondeana. Kila mtu alihisi huzuni wa Mlima Olokwango.

Watu wa Kwere wakachukua hatua. Wakamtoa Matata kisha wakamweka Baraka.

Baraka akaamrisha kila mtu kupanda ua kuuheshimu Mlima Olokwango. Wakasherehekea kwa kutolea Olokwango zawadi za msonobari, mwerezi na muhuhu.

Hakuna aliyetembea juu ya mlima tena, na nyasi zikamea na kuwa ndefu tena. Polepole, tabasamu iliyokuwa usoni mwa Mlima Olokwango ilipanuka zaidi na vibonyeo vikarefuka zaidi.



Kutoka kwenye vibonyeo, vijito vilitiririka tena.

Mto Temu ulifufuliwa.

Sehemu tambarare ziligeuka kijani zaidi ya hapo awali.

Paa walitembea tena kwa furaha kutoka upande mmoja hadi mwingine wakila nyasi.



"Maisha marefu, Baraka! Maisha marefu, Baraka!" Watu wa Kwere waliimba.

"Maisha marefu, Olokwango," Baraka na watu wake walisema. "Heri watoto wetu na watoto wa watoto wao wakuheshimu daima."

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Uamsho wa furaha

Author - Rebecca Njuguna
Translation - Brigid Simiyu
Illustration - Catherine Groenewald
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org



Wakati basi kubwa la bluu lilipochelewa

Ursula Nafula

Mango Tree

Kiswahili

African Storybook.org

Mara moja kwa siku, basi kubwa la bluu husimama katika kijiji cha akina Bobo kuwasafirisha watu hadi mjini. Bobo hajawahi kuliona basi kubwa kama hilo. Anayahesabu madirisha 9 ya abiria na moja la dereva. "Lazima kuna safu 9 za viti vya abiria, kila safu ikiwa na takriban viti 8," Bobo anawaza.

Ikiwa ni sawa namna Bobo anavyowaza, je, basi kubwa la bluu linaweza kuwabeba abiria wangapi?

Kesho, mamake Bobo atampeleka mjini kununua sare mpya ya shule. Mama huuza mayai dazeni moja kwa shilingi 120. Karibu kila juma, yeye hupata jumla ya shilingi 3600. Je, ni mayai dazeni ngapi anazohitaji kuuza ili aweze kupata shilingi 3600? Kwa majuma 4 yaliyopita, aliweka akiba nusu ya fedha zake ili amnunulie Bobo sare mpya.

Je, unaweza kufanya hesabu ya kiasi cha fedha alizoweka akiba kwa muda wa majuma 4?

Takriban miezi mitatu imepita tangu Bobo asafiri kwa basi. Ana hamu kubwa ya kutaka kusafiri tena!

Kesho itakuwa siku kubwa. Inapofika saa moja jioni, Bobo yuko kitandani, lakini hapati usingizi wowote. Hafikirii jambo jingine ila tu safari yake ya kwenda mjini. Ni saa tatu na nusu, lakini Bobo bado hajalala.

Kila asubuhi, mama humwamsha Bobo saa moja. Lakini leo, Bobo tayari yuko macho inapofika saa kumi na mbili, ingawa usiku uliopita, aliweza tu kulala ilipotimia saa tano.

Inapotimia saa moja, Bobo ameoga na kuvaa, tayari kuondoka. Je, Bobo alipata usingizi kwa saa ngapi usiku uliopita?

Saa moja kasororobo asubuhi, Bobo na mamake wanawasili kituoni. Lile basi kubwa la bluu linastahili kuwasili kituoni inapotimia saa mbili asubuhi.

Mamake Bobo anaitazama saa yake. Lile basi kubwa la bluu tayari limechelewa kwa dakika kumi na tano. "Lakini, kawaida, basi hili halichelewi. Sijui kuna shida gani?" mama anasema.

Muda mfupi baadaye, watu zaidi wanajiunga nao pale kituoni. Wao pia wanazitazama saa zao na kuuliza kwa nini basi limechelewa. "Sasa tayari zimetimia saa tatu. Nitachelewa kufika kazini!" mwanamume mmoja aliyevalia suti nyeusi, anasema.

Bobo na mamake ndio waliosubiri kwa muda mrefu zaidi. Bobo anaona kama amesubiri kwa saa nyingi. Lakini, si saa nyingi. Je, wamekuwa wakisubiri kwa muda gani?

Bobo ana wasiwasi. "Je, nitaipata sare yangu kweli?" anamwuliza mamake.

Bobo anahesabu kwamba safari ya kwenda mjini na kurudi itawachukua saa 4. Saa 1 kufika huko, saa 2 kununua na saa 1 kurudi nyumbani. "Kuna mpira wa soka saa nane ambao mimi na marafiki zangu tumepanga kucheza. Basi lisipofika kwa wakati, nitachelewa kujiunga na wenzangu kwa mchezo huo."

Bado wanasubiri. Bobo sasa analia. Watu wawili walio kwenye foleni, wanaondoka na kurudi nyumbani. Wengine wanaendelea kuzitazama saa zao.

"Hebu tuwe na subira. Nina hakika kwamba basi litakuja hivi karibuni," mamake Bobo anawaambia. "Ninataka kwenda nyumbani!" Bobo analia kwa sauti. Mamake anamtuliza, "Tusubiri kwa dakika kumi tu. Basi lisipokuwa hapa saa tatu na nusu, tutaenda nyumbani."

Halafu, wanasikia mngurumo wa basi barabarani. "Si niliwaambia," mamake Bobo anasema. "Sasa ni saa tatu na nusu kamili. Tutanunua kwa haraka. Basi likiondoka mjini kwa wakati, tutafika nyumbani kwa wakati ufaao nawe utacheza mpira wa soka ulivyopanga."

Bobo anafuta machozi. Anahisi uchungu miguuni. Amechoka. Hawezi kusubiri kuliabiri lile basi.

La kushangaza ni kwamba, basi hili sio lile kubwa la bluu. Bali ni basi ndogo nyekundu. Bobo anahesabu madirisha ya abiria 4 pekee kisha anasema, "Mama, basi hii ni ndogo sana kuliko lile la bluu. Halitakuwa na nafasi ya kutosha kuwabeba watu wote wanaokwenda mjini."

Je, unakubaliana na Bobo? Unaweza kukisia idadi ya abiria ambao basi hiyo ndogo itaweza kubeba?



Mamake Bobo anamtania, "Wasiwasi wako hauna msingi. Angalau sote tunaosubiri hapa kituoni, tutapata nafasi ya kuketi."

"Hebu tuabiri kwa haraka ili tupate viti vizuri. Tumekuwa tukisubiri kwa muda mrefu zaidi ya wote!"

Bobo na mamake wanaabiri basi. Nyuma yao kuna watu 9 zaidi wanaotaka kuabiri. "Je, kutakuwa na viti vya kututosha sote?" Bobo anauliza.

Anaona kwamba kuna safu 4 za viti basini, upande mmoja ukiwa na viti 2 na mwingine ukiwa na viti 2 pia. Je, kuna viti vingapi jumla? Je, watu wote walio kwenye foleni wataweza kuketi?



Bobo na mamake wanakalia viti 2 vilivyo mbele karibu na mlango. Wana nafasi kubwa mbele yao na pia wanaweza kutazama nje vizuri.

Bobo anahesabu watu 6 wapya wanaojiunga na wengine kwenye foleni. "Hao wanafanya jumla ya idadi ya abiria kuwa 17," anawaza. "Mama, kuna nafasi ya kila mtu," Bobo anamweleza mamake. "Ni mtu mmoja tu atakayelazimika kusimama."

Je, Bobo alihesabu sawa?

Basi sasa imejaa. Dereva anaifunga milango na kuanza safari. Kuna kelele nje. Bobo na abiria wengine wanatazama dirishani.

Watu zaidi wanakimbia wakitaka kuifikia basi. Wanapiga mayowe, "Subiri! Subiri! Tunahitaji usafiri." Lakini wamechelewa. Bobo na mamake wanawahurumia walioachwa nyuma.



Mamake Bobo anamwuliza dereva, "Mbona hukujia lile basi kubwa la bluu?" Dereva anajibu, "Liliharibika jana. Hii basi ndogo nyekundu pekee ndiyo iliyopatikana."

"Je, na wale watu wote tuliowaacha nyuma?" mamake Bobo anauliza. Dereva anasema, "Usiwe na wasiwasi. Nitakuwa na safari mbili leo."

Bobo anasikiliza wanavyozungumza. Mawazo yake yanajaa nambari.

Bobo anahesabu viti tena. "Basi hii inawabeba watu 20, 16 wakiwa wameketi na 4 wakiwa wamesimama." Anajiuliza, "Basi hii itaweza kwenda safari ngapi ili iwapeleke abiria 100 mjini? Na abiria 200 au 150, je?" Unaweza kulipata jawabu?

Bobo amefurahi. Hivi karibuni, ataipata sare mpya. Kisha, basi itawarudisha nyumbani kwa wakati ili acheze soka.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Wakati basi kubwa la bluu lilipochelewa

Author - Mecelin Kakoro
Translation - Ursula Nafula
Illustration - Mango Tree
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2015
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org



Wanamuziki stadi

Ursula Nafula
Salim Kasamba

Kiswahili

African Storybook.org

Bul, Fumbo, Teke, Tongoli, Milege, Sos na Gwara walikuwa marafiki wakubwa. Pia waliimba muziki mzuri. Waliishi karibu na milima mashariki mwa Uganda. Wote walikuwa wanamuziki stadi. Kila mtu alifurahi kusikiliza nyimbo zao na kucheza kufuata mdundo wao! Hawa wanamuziki stadi walitaka kumchagua kiongozi wao. Aliyetambuliwa kwa umaarufu wake zaidi ya wote, ndiye angekuwa mfalme wao.

Ili kuchaguliwa kama mfalme, kila mwanamuziki alitakiwa kudhihirisha kwamba anaweza kusikika na walio karibu na vilevile walio mbali. Tongoli aliongea kwanza, "Mimi ni mfalme. Ninaimba sauti ya juu na
vilevile ya chini. Nina nyaya nyingi zenye milio tofauti. Ninaweza kuimba peke yangu na pia katika kikundi. Vijana kwa wazee hupenda kucheza muziki wangu. Hata ninamwongoza Fumbo kwenye nyimbo."

"Ulivyosema ni ukweli Tongoli," Fumbo alikubali. "Lakini, wewe hunishindi mimi. Sauti yako ni laini sana. Mimi nina sauti kubwa iliyo wazi na inayofika karibu na mbali." Fumbo aliendelea, "Watu hucheza muziki wangu mpaka karibu wavunjike migongo! Iwe wakati wa furaha au wa majonzi, mimi huwafanya watu wacheze! Watoto hupenda kuiga midundo yangu."



"Nyote wawili ni viongozi," Milege alikubali kisha akaendelea, "Kazi yangu ni rahisi. Wachezaji hunifunga vifundoni. Wanapoitikisa miguu yao kwa mdundo, mimi hutoa muziki wa kupendeza. Ninatoa mchanganyiko wa sauti za juu na zinazokwaruza. Je, mimi si kiongozi?"

"Hiyo ni sawa!" Bul alisema. "Mimi nimetengenezwa
kutoka kipande cha ngozi kilichowambwa juu ya mti ulio na uwazi. Mimi hutia midundo kwenye nyimbo na sauti yangu hutambulisha vitu vingi. Lakini siwezi kubadilisha sauti yangu kama mnavyofanya ninyi. Sidhani kama mimi ninaweza kuwa kiongozi."

"Bul, wewe hutenda mambo makuu!" Gwara alitofautiana naye. "Wewe huwaita watu kwenye mikutano, ibada, na kazi za kijamii na pia hutangaza vifo na kuwatahadharisha watu kunapokuwa na hatari. Unasikika wakati wa sherehe na kuwafanya watu wacheze kwa furaha na kwa huzuni. Kulingana nami, wewe ni mkubwa zaidi." Gwara alitoa mlio mkubwa na kusema, "Mimi nina sauti kubwa tena ninawavutia watu. Hata hivyo, mimi si bora kumliko Bul. Ninapendekeza yeye awe mfalme."

Wanamuziki hao stadi walitazamana kwa mshangao wakabaki kimya. Kisha Tongoli akasema, "Bul ni mtu wa kawaida sana, hawezi kuwa mfalme. Mimi ndiye mkubwa zaidi kwa sababu ninacheza kuanza kwa sauti ya chini hadi ya juu zaidi bila tatizo lolote." Sos ambaye alikuwa kimya wakati huo wote, sasa aliongea, "Marafiki, mimi nimekuwa nikiimba nanyi nyote. Nyote ni wanamuziki stadi. Lakini, ni bora tumchague Bul kuwa mflame wetu."



Sos aliendelea, "Mtu asiyesikia muziki unaoimbwa na Bul ni kama gogo lililokufa! Bul huwavutia watu kwake na kuwaliwaza kwa muziki wakati wa huzuni na kuwaburudisha wakati wa furaha." Mwishowe, wanamuziki hao stadi walimchagua Bul kuwa mfalme wao. Tangu wakati huo, Bul amekuwa mfalme wa muziki. Hiyo ndiyo sababu Bul yuko katika kila nyumba ya jamii inayoishi milimani mashariki mwa Uganda.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Wanamuziki stadi

Author - Athieno Gertrude and Owino Ogot
Translation - Ursula Nafula
Illustration - Salim Kasamba
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2017
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org



Wanyama hushukuru

Susan Kavaya
Rob Owen

Kiswahili

African Storybook.org



Hapo zamani za kale, Binadamu, Simba, Punda, Nyoka, Tai, na Mbwa walikuwa wamekwenda vitani pamoja. Walisafiri siku nzima hadi jua lilipotua.

"Tutalala wapi?" Punda aliuliza.

"Tazameni, ninaona moshi ukitoka katika nyumba ile. Tunaweza kulala huko," Nyoka alisema.



Walipobisha, mtu na mkewe walitoka nje. Nyoka aliuliza, "Tunaweza kulala kwenu?" Waliwajibu, "Tunawakaribisha mlale, lakini, hatuna chakula cha kuwapa."

Mbwa alisema, "Tulimwona ng'ombe wenu."

Mume alijibu, "Huyo ng'ombe pekee ndiye tuliye naye. Tukimchinja, tutabaki bila chochote."

Binadamu na wanyama walisema, "Tutawalipa. Tafadhali, tuchinjie ng'ombe wenu."



Simba alisema, "Naomba damu. Nitakupa zawadi siku moja." "Nipe mifupa. Nitakuletea zawadi pia." Mbwa alisema."

Binadamu alisema, "Nipe maziwa. Nitakupa zawadi maalum."

Nyoka akasema, "Nipe mafuta. Hutajuta." "Naomba vipande vya sarara. Nitakupa zawadi pia," alisema Tai.

Punda naye alisema, "Mimi nipe nyasi kutoka paa la nyumba yako. Siku moja utanishukuru."

Mtu na mkewe walimchinja ng'ombe wao wa pekee.

Wakampa Simba damu, Mbwa akapewa mifupa, Binadamu akapewa maziwa, Nyoka akapewa mafuta, na Tai akapewa vipande vya sarara. Punda naye akapewa nyasi kutoka paa la nyumba.

Wageni wale walilala vizuri usiku ule.

Asubuhi kulipokucha wakaenda zao.

Baada ya wiki nyingi, mtu huyo na mkewe walimsikia Simba akinguruma karibu na nyumba yao. Walipotoka nje, hawakumpata Simba, lakini, kulikuwa na pembe ya tembo iliyolazwa nyasini.

"Pembe hii ni ya thamani. Ipeleke ndani. Lazima tuwe waangalifu wezi wasije kuiiba," mume alimwambia mkewe.

Ghafla, yule mtu na mkewe wakatazama nyuma yao. Walimwona Mbwa amelala karibu na mlango wa nyumba yao.

Alisema, "Msiwe na wasiwasi. Nitawazuia wezi wasiingie nyumbani kwenu. Nakumbuka mlinisaidia na sasa wacha niwasaidie pia."

Yule mtu alikuwa na kaka. Kakake huyo alikuwa tajiri, lakini, alikuwa mwovu na watu wote walimchukia.

Alipopata habari kuhusu pembe ya tembo, aliwaza, "Ninaitaka pembe ile. Nitamuua kakangu halafu niichukue."

Usiku wa manane, alikwenda nyumbani kwa kakake.

Nyoka mkubwa alikuwa amelala karibu na mlango wa nyumba ya mtu yule na mkewe.

Nyoka huyo alimuuma kaka mwovu akaaga dunia.

Katika nchi ile, mtu alipokufa, mali yake ilirithiwa na kakake. Kwa sababu hiyo, ng'ombe na kondoo wa kaka mwovu walirithiwa na kakake aliyekuwa hai.

Yule mtu alimwambia mkewe, "Simba, Mbwa, na Nyoka wametulipa vizuri. Tai, Punda, na Binadamu watafanya nini?"

Siku moja, Tai alipokuwa akiruka juu angani, aliwaona wazee wakitembea pamoja barabarani. Mikononi mwao walikuwa na kitu fulani kilichong'aa sana.

"Nadhani wana pesa na vito. Inaonekana wanampelekea mume zawadi kutoka kwa mkewe au kutoka kwa mume kwenda kwa mkewe ili kumaliza ugomvi. Mwishowe, watasameheana tu." Tai aliwaza.



Tai aliruka chini akazichukua zile zawadi kutoka mikononi mwa wazee.

Aliziangusha zawadi hizo nje ya nyumba ya yule mtu na mkewe waliomsaidia mbeleni.

Siku hiyo, Punda alikuwa katika msitu uliokuwa karibu. Mgongoni, alikuwa amebeba mfuko mzito uliojaa pesa. Bwana wake alimpiga akisema, "Enda kasi au nikuue! Wewe mnyama mpumbavu na mvivu!"

Punda huyo aliwaza jinsi angemwadhibu bwana wake mwovu.

Punda alitoroka akaenda nyumbani kwa yule mtu na mkewe akwaambia, "Chukueni pesa hizi. Ni zawadi yenu."

Yule mtu na mkewe walitajirika kutoka siku ile.

Mtu yule alisema, "Rafiki zetu, wanyama, wamekuwa wema sana kwetu. Ilikuwa vyema kwamba tulimchinja ng'ombe wetu wa pekee tukawapa."

Mkewe alimjibu, "Lakini, Binadamu hajatupa zawadi yoyote. Hakika, wanyama wametufanyia mambo mengi. Ninajua Binadamu atatufanyia mambo mazuri zaidi."

Walingoja, wakangoja. Wiki nyingi zikapita, kisha miezi na miaka, lakini Binadamu hakurudi.

Wanyama wote walitimiza ahadi zao.

Binadamu alisahau.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Wanyama hushukuru

Author - Mariam Mohammed and Elizabeth Laird
Translation - Susan Kavaya
Illustration - Rob Owen
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© African Storybook Initiative 2016
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org
Original source www.ethiopianfolktales.com



Zawadi ya Sisanda

Ursula Nafula

Kiswahili

ASb approved

Sisanda ni msichana wa umri wa miaka minane. Kila siku anapotoka shule, anavua sare, anakula chakula cha mchana kisha yeye na babu yake wanacheza mchezo waupendao. Wanafurahia sana kucheza hadi Sisanda hataki kuacha.

Babu anamkumbusha kuwa angependa kuwa meneja wa benki atakapokuwa mkubwa.

Babu anamwuliza kwa utani, "Utawezaje kuwa meneja wa benki usipokwenda shule ya upili?"

Sisanda anacheka tu. "Nitamaliza masomo ya shule ya upili na hata niende chuo kikuu. Hiyo ndiyo sababu ninatia bidii sana masomoni!"

Sisanda ni mrefu kwa umri wake. Anafuata urefu wa babake. Anamfanana mamake kwa uso wake ulio mfiringo na kwa tabasamu yake. Kila siku wazazi wake huamka mapema na kwenda wanakofanya kazi kwenye hifadhi ya wanyama iliyo karibu.

Wakati Sisanda na rafiki zake wanapoanza kwenda shule, mabasi huwa tayari yamewafikisha watalii kwenye hifadhi hiyo ya wanyama.



Maadhimisho ya kuzaliwa kwake iliyopita, Sisanda aliandaliwa sherehe maalum. Wazazi walipata ruhusa ya kuandaa sherehe hiyo katika hifadhi ya wanyama. Twiga walivutiwa sana na watu waliofika kwa sherehe hiyo. Waliyanyoosha mashingo yao marefu wakaiona sherehe vizuri na kutaka kuptata sehemu ya keki! Sisanda aliwapenda twiga zaidi ya wanyama wote kwa ajili ya upole na utulivu wao. Angewatazama kwa siku nzima.

Ijumaa moja, babake Sisanda alikuja nyumbani mapema kutoka kazini. Alionekana kuwa mwenye hasira. Sisanda alimwuliza, "Baba, kuna nini kibaya?"

Babake alieleza, "Leo, kundi la nyuki lilimuuma mama twiga. Kichwa chake kilivimba hadi macho yake ya kupendeza yakazibwa. Tulijaribu kumwokoa, lakini ilikuwa bure. Alikufa. Kinachohuzunisha zaidi ni kwamba alikuwa na ndama mchanga ambaye bado anamhitaji."

"Ah, la!" Sisanda alianza kulia. "Heri ningeweza kumsaidia. Labda yule ndama vilevile analia kama mimi." Sisanda alilia kwa muda mrefu. Mamake alijaribu kumfariji. Alimsomea hadithi moja zaidi wakati wa kulala ili aweze kusahau angalau kidogo uchungu aliokuwa nao kumhusu yule ndama. Hatimaye, Sisanda alipatwa na usingizi huku akisikiliza sauti ya mamake.

Asubuhi iliyofuata Sisanda alikuwa na wazo! Alimwuliza babake, "Ninaweza kwenda kufanya kazi nawe leo? Ningependa kumpelekea mtoto twiga zawadi."

Wazazi wake walitazamana kisha wakatabasamu, "Ndiyo, bila shaka, unaweza kuja nasi."

Siku hiyo ilikuwa yenye joto na mawingu. Kila kitu katika hifadhi ya wanyama kilitulia. Sisanda alisema, "Nadhani hakuna jua leo kwa sababu ya huzuni wa mtoto twiga."

Tembo mkubwa aliitazama familia hiyo ikipita. Mamake Sisanda alisema, "Labda anashangaa kwa nini msichana mdogo anaenda kufanya kazi na wazazi wake." Sisanda aliitkia kwa kichwa. "Atashangaa atakapogundua," Sisanda aliwaza.



Walimpata mtoto twiga akiwa peke yake. Alilegeza shingo lake refu na kuinama. Macho yake makubwa yalipumbaa. Sisanda alisimama aliufungua mkoba wake akatoa kitabu. Wazazi wake walishangaa alipoanza kumsomea mtoto twiga. Mtoto twiga aligeuza kichwa chake akatazama kulikotoka sauti ya Sisanda akasikiliza kama aliyelewa kila neno. Mwanzoni, wazazi walidhani kumsomea twiga ni jambo la ajabu, lakini walibadili mawazo yao walipomwona mtoto twiga akitulia.

"Hadithi yangu ilimfariji," Sisanda alimwambia babu yake alipofika nyumbani. Sisanda alienda kumtembelea mtoto twiga kila alasiri na wakati wa wikendi.

Kila alipoenda, alibeba hadithi tofauti kumsomea. Marafiki hao wawili walionekana vizuri pamoja hata watalii waliopita waliwapiga picha.

Polepole, mtoto twiga alianza kupata nguvu. Watu waliofanya kazi katika hafidhi hiyo walimlinda vizuri. Upendo kutoka kwa rafiki yake Sisanda, ulifanya miujiza.

Siku moja meneja wa hifadhi alimwuliza Sisanda ampatie rafiki yake mpya jina. "Furaha ni jina nzuri," Sisanda alisema.

Siku iliyofuata meneja wa hifadhi alimpigia simu mwalimu wa Sisanda. Akawaalika wanafunzi wa darasa la Sisanda kumtembelea Furaha.

Mtoto twiga alikuwa amekua mrefu na mwenye nguvu katika muda wa miezi mitatu tangu Sisanda alipomtembelea mara ya kwanza.



Siku ya matembezi, wanafunzi 40 wa darasa la 3 walisubiri kwa hamu kufunguliwa kwa lango la hifadhi. Sisanda aliwaongoza wote wakaenda kumwona Furaha. Wengine walimtazama yule twiga mrefu kwa mshangao. Wengine walicheka kwa woga. Mwalimu wao, Bi Keziah, alitabasamu tu.

"Sisanda, rafiki yako ni mrembo. Umemsaidia sana," mwalimu alisema. "Anaitwaje?" Mvulana mmoja aliuliza. "Anaitwa Furaha," Sisanda alimjibu. Bi Keziah alisema, "Bila shaka anafurahi."

Watoto waliketi chini wakamsikiliza Sisanda akisoma hadithi aliyomsomea Furaha siku aliyomtembelea mara ya kwanza. Meneja wa hifadhi alipiga picha. Baadhi ya watalii waliopita pia walipiga picha.

Mpiga picha kutoka gazeti moja vilevile alipiga picha. Aliwaahidi kuwa picha yao ingechapishwa katika gazeti la mtaa wao hivi karibuni. Kila mmoja alishangilia.

Ilikuwa zawadi ya kipekee! Sisanda kusoma hadithi ili kumponya rafiki.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Zawadi ya Sisanda

Author - Gcina Mhlophe
Translation - Ursula Nafula
Illustration -
Language - Kiswahili
Level - Read aloud

© Text: Gcina Mhlophe; Illustrations: Jiggs Snaddon-Wood 2015
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org